SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



UKURASA 2

**WAZIRI** kuongoza watu 300 kupanda Mlima Kilimanjaro




UKURASA 11

Nipashe
Jumatatu Novemba 22, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580772
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Nyumba zote maeneo hatarishi kubomolewa

**ZIMO** za mabondeni, ubomoaji hautajali hatimiliki ya viwanja...

*Endelea ukurasa wa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro kwa ziara ya kikazi ya siku tatu.
**PICHA: IKULU**

## DPP aitisha jalada kesi ya kughushi cheti cha ndoa

UKURASA 3

# Mapenzi ya jinsia moja, ukahaba tishio Zanzibar

UKURASA 17

**MICHEZO** LIGI KUU YAREJEA NA REKODI ZA KUMWAGA UK.14
**MAONI, KATUNI** UK.6



Mhandisi wa Mradi wa Mwalimu Julius Nyerere, Lutengano Mwandomba, akiwaelekeza Bodi ya Makandarasi (CRB) namna ya bwawa hilo la kuzalisha umeme litakavyokuwa eneo walipofanya ziara ya kutembelea mradi huo mwishoni mwa wiki, (wanne kushoto) ni Mwandisi Consolatha Ngimbwa na (wapili kulia) ni Msajili wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Rhoben Nkori. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Nyumba zote maeneo hatarishi kubomolewa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amesema serikali itavunja nyumba zote ambazo zimejengwa katika maeneo hatarishi na mabondeni bila kujali kuwa wamiliki wake wana hati miliki za viwanja.

Luvuvi, alibainisha hayo jana jijini hapa wakati alipokuwa akitoa taarifa ya mafanikio ya sekta ya ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi kwa waandishi wa habari katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika.

Alisema kwa mujibu wa sheria wananchi hawaruhusiwi kujenga katika maeneo hatarishi pamoja na mabondeni na kwamba yeyote atayekaidi serikali itabomoa bila kujali kuwa anayo hati miliki ya kiwanja chake.

"Miaka ya nyuma fedha ilikuwa na nguvu kuliko sheria hali ambayo ilifanya hata watumishi wa wizara yetu kutoa hati katika maeneo hatarishi na mabondeni kama vile bonde la mto Msimbazi," alisema Lukuvi. Vilevile, alisema serikali ipo kwa ajili ya kulinda wananchi wake na hatokuwa tayari kuacha watu kujenga katika maeneo hatarishi na kwenye mabonde.

"Kama kuna mtu amejenga katika eneo hatarishi tukigundua tunakuvunjia bila kujali kuwa unayo hati maana yake kuna baadhi ya hati watu wamepatiwa kiujanjaujanja bila kufuata taratibu ndiyo maana unakuta watu wanajenga katika maeneo kama vile bonde la Msimbazi," alisema Lukuvi. Kutokana na hali hiyo aliwaagiza watumishi wa wizara hiyo kuacha kufuata hisia za watu kwenye utoaji wa hati katika maeneo hatarishi na mabondeni. "Ukipewa hatimiliki ya eneo katika maeneo hatarishi na kwenye mabonde imekula kwako kwani tukibaini tu lazima tukuvunjie," alisisitiza Lukuvi.

Akizungumzia kuhusu malalamiko yanayotolewa hivi sasa na wananchi kuhusu malipo ya fidia ya maeneo yao yaliyochukuliwa na serikali kwa ajili ya kupisha miradi ya kimkakati kama wa SGR, alisema suala la fidia sio hisani ni lazima kwa mujibu wa sheria. Alizitaka taasisi zote za serikali zilizochukua maeneo ya wananchi kwa ajili ya miradi mbalimbali kuhakikisha kuwa zinawalipa fidia kwa mujibu wa sheria.

"Suala la kulipa fidia siyo hisani ni lazima kwa mujibu wa sheria kwani sheria inasema kuwa ukimcheleweshea mtu malipo yake ya fidia ndani ya miezi sita unatakiwa kumlipa na riba na ukichelewa kwa miaka miwili tathmini inabidi ifutwe na ifanyike nyingine hivyo wahakikishie watu wote ambao wamepitiwa na miradi ya umma kuwa watalipwa," alisema Lukuvi.

Kadhalika alisema hivi sasa serikali imetoa Sh. bilioni 50 kwa halmashauri nchini kwenda kufanya upimaji wa ardhi pamoja na upangaji wa miji ili kuwezesha wananchi kupata hatimiliki za maeneo yao.

## Reli iliyofukiwa kwenye kiwanda sasa yafukuliwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

UONGOZI wa Kiwanda cha Kiluwa kinachozalisha nondo umeanza kufukua reli iliyokuwa imefukiwa na udongo, hivyo kukwamisha kazi ilivyolengwa wakati wa ujenzi wake.

Kazi ya kufukua reli hiyo imeanza baada ya ziara ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, hivi karibuni, ambaye pamoja na kufika kwa ajili ya kupata taarifa ya hali ya uzalishaji wa nondo, alikagua reli iliyojengwa na serikali kiwandani hapo kwa ajili ya kusafirisha bidhaa na malighafi.

Akiwa kiwandani hapo Majaliwa alishuhudia reli hiyo iliyojengwa kwa ajili ya kurahisisha usafiri wa bidhaa zinazozalishwa, ambapo pia reli hiyo ilionekana kutotumika, huku ikiwa imefukiwa kwa udongo, kitu kilichomkasirisha.

Kufuatia hali hiyo, Majaliwa aliahidi kupeleka timu katika kiwanda hicho mbali ya kuchunguza vitu vingine, pia ichunguze sababu za reli hiyo kutotumika, ingawa wamiliki wa kiwanda hicho ndio waliomba ijengwe.

Siku chache baadaye Nipashe ilifika katika kiwanda hicho na kushuhudia shughuli ya kufukua reli ikielekea ukingoni, huku pia ukuta uliokuwa umejengwa juu ya reli hiyo ukiwa umeshavunjwa.

Akizungumzia kuhusiana na hali hiyo, Meneja Mwajiri wa Kiluwa, Mohamed Kimea, alisema reli hiyo ilifukiwa na udongo kutokana na kutotumika kwa muda, lakini baada ya ziara Majaliwa imefukuliwa katika maeneo yote yaliyokuwa yameziba, huku akiahidi hali hiyo kutojirudia.

Naye Anyandwile Shibanda, mfanyakazi wa kiwanda hicho, alisema baada ya kukamilika kwa ufukuaji wa reli hiyo, watakuwa mabalozi wazuri katika utunzaji wa miundombinu inayojengwa na serikali.

## Waziri kuongoza watu 300 kupanda Mlima Kilimanjaro

**Na Sanula Athanas,** ARUSHA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, amesema atakuwa miongoni mwa Watanzania takriban 300 wanaotarajiwa kupanda Mlima Kilimanjaro kuadhimisha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Arusha jana, Dk. Ndumbaro alisema wizara hiyo kushirikiana na kampuni ya kitalii ya ZARA, katika kusherehekea miaka 60 ya uhuru, inaratibu upandaji wa mlima huo kwa gharama nafuu ya Sh. 800,000 kwa kila mpandaji.

Gharama za kuupanda Mlima Kilimanjaro kwa Mtanzania ni wastani wa Sh. milioni 1.5.

"Mpaka sasa (jana asubuhi) watu 120 wameshajisajili kuupanda mlimani wetu kupitia kampuni ya ZARA Tours inayoshirikiana na wizara kuendesha kampeni hii," alisema. Waziri Ndumbaro alifafanua njia itakayotumika ni ya Marangu ambayo ukomo wake ni watu 120. Kadri watu watakavyoongezeka, tutawapeleka kwenye njia nyingine."

Alipoulizwa kuhusu mpango wa kuanza kutumia 'cable car' kupanda Mlima Kilimanjaro, Dk. Ndumbaro alisema suala hilo ni fursa kwa wawekezaji kutoka sekta binafsi.

"Kazi ya kupandisha watalii mlimani inafanywa hasa na sekta binafsi, serikali ipo pale kuratibu masuala ya yaende vizuri kwa utaratibu unaotakiwa.

"Kama sekta binafsi wanaona kuna fursa ya kutumia 'cable car' kupanda Mlima Kilimanjaro, wachangamkie fursa hiyo," alisema.

Dk. Ndumbaro alisema upandaji wa Mlima Kilimanjaro kuadhimisha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika utaanza Desemba 5 mwaka huu, ili inapotimu Desemba 9 (siku ya uhuru), wapandaji wawe tayari wamefika kileleni.


IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

TEMEKE HIGH COURT SUB – REGISTRY
(ONE STOP JUDICIAL CENTRE)
AT TEMEKE

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 36 OF 2021

In the Matter of the Estate of the Late FERDINAND JOSEPH MPANDUJI

and

In the Matter of Application for Letter of Administration of the Late FERDINAND JOSEPH MPANDUJI DECEASED OF DAR ES SALAAM

By OIGENIA FREDINAND MPANGUJI……….PETITIONER

GENERAL CITATION
(Rule 75)

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above-named petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 8th day of December, 2021.
Dated at this 18th day of November, 2021.

DEPUTY REGISTRAR

116580002



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KUITWA SHAURINI MDAIWA
MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU
WILAYA YA GEITA
SHAURI LAMADAI NAMBARI 191/2021
MDAI: WILLYBROAD SAMSON KASHAMBA

DHIDI YA
MDAIWA GOLDBED CO.LTD
WA
BARA NA VISIWANI

AMRI:
Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakamani mnamo tarehe 23/11/2021 Saa 2:30 Asubuhi bila kukosa.
Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo,na kutolewa uamuzi.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo Jumanne tarehe

PRIMARY COURT MAGISTRATE
HAKIMU GEITA

# DPP aitisha jalada kesi kughushi cheti cha ndoa

**Na Kulwa Mzee**

MKURUGENZI wa Mashtaka nchini (DPP) ameitisha ofisini kwake jalada la kesi ya kughushi cheti cha ndoa inayomkabili Khairoon Jandu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Kesi hiyo iliyotakiwa kuanza kusikiliza ushahidi wa upande wa mashtaka inasikilizwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Joseph Luambano.

Wakili wa utetezi, Abubakar Salim mara kadhaa alikuwa hafiki mahakamani kwa ajili ya kesi kuendelea na DPP aliamua kuliitisha jalada la kesi hiyo ofisini kwake.

Kesi hiyo ambayo upelelezi wake ulishakamilika muda mrefu na mashahidi kuandaliwa kwa ajili ya kuanza kutoa ushahidi wao, ilikwama mara kadhaa na kuahirishwa mpaka Novemba 29, mwaka huu ili kuangalia kama DPP atakuwa amerejesha jalada la kesi hiyo mahakamani hapo ama la.

**"Mheshimiwa hakimu pamoja na wakili kuleta taarifa hii, lakini naona kuna mchezo anafanya hii ni mara ya tano sasa kesi inashindwa kuendelea kwa yeye kutofika mahakamani, naandaa mashahidi lakini wakili haonekani mahakamani,"**

Awali, kesi hiyo ilipangwa kuanza kusikilizwa kwa mfululizo kuanzia Novemba 1 hadi 3, mwaka huu na miongoni mwa mashahidi ni wakili wa kujitegemea, Jerome Msemwa.

Awali, kabla ya jalada la kesi hilo kuitishwa kwa DPP ilikwama kuanza kusikilizwa kwa sababu Wakili wa Utetezi, Salim alikuwa anahudhuria kesi Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi.

Baada ya taarifa hiyo Wakili wa Serikali Ashura Mzava alimlalamikia wakili huyo wa utetezi akidai ni mara ya tano sasa kesi hiyo inashindwa kuendelea kutokana na yeye kutofika mahakamani.

"Mheshimiwa hakimu pamoja na wakili kuleta taarifa hii, lakini naona kuna mchezo anafanya hii ni mara ya tano sasa kesi inashindwa kuendelea kwa yeye kutofika mahakamani, naandaa mashahidi lakini wakili haonekani mahakamani," alidai wakili Mzava.

Katika kesi hiyo Khairoon anadaiwa katika tarehe na mwezi usiofahamika mwaka 2020, jijini Dar es Salaam kwa njia ya udanganyifu alighushi cheti cha kuzaliwa cha mtoto Gurditsing Jandu, akionyesha kuwa kimetolewa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) wakati akijua kuwa ni uongo.

Katika shtaka lingine, Khairoon anadaiwa kuwa katika tarehe na mwezi usiofahamika mwaka 2020 alighushi cheti cha ndoa akionyesha kimetolewa na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania Bakwata jambo alilojua kuwa sio kweli.

# Mgombea ACT Ngorongoro aanika vipaumbele vyake 5

**Na Thobias Mwanakatwe, NGORONGORO**

MGOMBEA ubunge Jimbo la Ngorongoro mkoani Arusha kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Johnson Mahuma, amesema iwapo atapata ridhaa ya kuongoza, atashughulikia kero tano ikiwamo ya kuhakikisha wafugaji hawahamishwi ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Akizungumza katika mahojiano maalum na gazeti hili, alisema jimbo hilo linakabiliwa na changamoto nyingi, na kwamba ameamua kugombea ili aweze kuzitatua ndani ya kipindi kifupi.

"Hivi sasa serikali ina mpango wa kuwahamisha wafugaji ndani ya hifadhi ambao wamekuwapo humo tangu 1960... huu mgogoro nikichaguliwa nitahakikisha hawaondolewi maana uwapo wao ndani kimekuwa ni kivutio kwa watalii," alisema.

Mahuma alisema wafugaji waliomo ndani ya hifadhi hiyo wamekuwa walinzi wazuri wa majangili, na kwamba hawana historia ya kufanya ujangili, hivyo kutaka kuwaondoa ni kuwaonea na atahakikisha anawapigania atakapokuwa mbunge.

Kero nyingine atakazozishughulikia akipata ridhaa ni kuboresha miundombinu kutokana na barabara nyingi katika jimbo hilo kutopitika hususani wakati wa masika, hali ambayo inawafanya wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro kufuata mahitaji yao nchi jirani, ambako miundombinu ni mizuri.

Kero ya tatu atakayoishughulikia migogoro ya ardhi ambapo baadhi ya wawekezaji wamechukua maeneo makubwa ya ardhi, hivyo kusababisha wananchi kukosa maeneo ya kuendesha shughuli za kilimo na ufugaji.

Mahuma alisema kero ya nne atakayoishughulikia akichaguliwa ni ukosefu wa mabwawa kwa ajili ya kunyweshea mifugo, ambapo atahakikisha yanajengwa ya kutosha kila tarafa ili kuwaondolea kero hiyo wafugaji.

Kero ya tano atakayoishughulikia ni usimamizi wa mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro ili yaweze kutumika kwa ajili ya kujenga vituo vya afya na kuboresha miundombinu ya elimu.

Alisema hivi sasa anaendelea na kampeni ambayo alianza Jumatano Orgosorok na Waso mjini.

Mahuma alisema uzinduzi rasmi wa kampeni wa chama chake utafanyika Novemba 29, ambapo watahudhuria viongozi mbalimbali wa kitaifa.


**CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE**

**MAHAFALI YA KUMI NA SITA (16) KAMPASI YA KIVUKONI NA MAHAFALI YA SITA (6) KAMPASI YA KARUME ZANZIBAR- 2021**

Mkuu wa Chuo anawatangazia wanafunzi waliohitimu masomo yao katika mwaka wa masomo 2020/2021 kwamba **Mahafali ya Kumi na SITA** yatafanyika kwenye Kampasi ya Kivukoni, siku ya **Ijumaa tarehe 26 Novemba, 2021** kuanzia **saa TATU ASUBUHI (03:00) na Mahafali ya Sita** katika Kampasi ya karume Zanzibar yatafanyika **Jumatatu tarehe 29 Novemba, 2021** kuanzia saa **TATU ASUBUHI.**

Wahitimu wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. Kuchukua Majoho kwenye ofisi namba 115 – Jengo la Uhuru **Kampasi ya Kivukoni kuanzia Jumatatu, tarehe 22 hadi Alhamisi, tarehe 25 Novemba, 2021 wakati wa saa za kazi na kwa Kampasi ya Karume - Zanzibar wafike Ofisi ya PMU kuanzia Ijumaa tarehe 25 hadi Jumapili tarehe 28 Novemba, 2021 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri. Majoho hayatatolewa siku ya mahafali.**
2. **MALIPO YOTE YA KULIPIA MAJOHO YALIPWE KWA KUTUMIA MFUMO WA KIELEKTRONIKI (CONTROL NUMBER)**
3. Majoho sharti yarejeshwe Chuoni kabla ya **tarehe 3 Desemba, 2021 kwa Kampasi ya Kivukoni na Kampasi ya Karume- Zanzibar.** Vinginevyo **faini ya shilingi 10,000/=** itatozwa kwa siku kwa yeyote atakayechelewa kurudisha joho hilo.
4. Zoezi la namna ya kupokea vyeti (**rehearsal**) litafanyika A**lhamis, tarehe 25 Novemba, 2021 kuanzia saa 6.00 mchana** katika uwanja wa Mahafali **Kampasi ya Kivukoni na kwa Kampasi ya Karume-Zanzibar zoezi hilo litafanyika Jumapili tarehe 28 Novemba, 2021 kuanzia saa 4:00 asubuhi katika uwanja wa mahafali. Mhitimu atakayeshindwa kuhudhuria zoezi hilo, hataruhusiwa kushiriki katika Mahafali hayo.**
5. Kila mhitimu atapaswa kujigharamia usafiri, malazi na chakula.
6. kusanyiko la wahitimu wote **(CONVOCATION)** waliosoma katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere litafanyika **Alhamis, tarehe 25 Novemba 2021** katika Ukumbi mpya wa Mihadhara **(NEW LT)** chuoni hapo kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa sita mchana.
7. Washiriki wote wa Mahafali wanatakiwa kuthibitisha ushiriki wao katika Ofisi ya Mitihani kabla ya tarehe **25 Novemba, kwa kupiga simu namba 0782405552**

**Nyote Mnakaribishwa.**

**Mkuu wa Chuo,**
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere,**
**S.L.P. 9193,**
**DAR ES SALAAM.**
**Simu: +255 22 2820041/ 2820045/ 2820047**
**Faksi: +255 22 2820816**
**Barua pepe: rector@mnma.ac.tz**

216573202

# Naibu Gavana ataja sababu Watanzania kupuuzia bima

**Na Christina Mwakangale**

VIWANGO vya juu vya malipo ya bima, elimu duni na uhaba wa upatikanaji wa huduma hizo vimetajwa kuwa kati ya sababu ya Watanzania kutoipa kipaumbele huduma hiyo ambayo ni muhimu kwenye sekta ya fedha nchini.

Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Bernard Kibesse, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam kwenye mahafali ya kwanza ya cheti cha umahiri wa Bancassurance katika Chuo cha Afrika cha Bima na Hifadhi ya Jamii, akimwakilisha Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Masuni Yusuf Masauni.

Alisema kutokuwapo kwa elimu kuhusu bima kumesababisha umma kushindwa kupata huduma, kuzingatia hata huduma zilizo za lazima ikiwamo za magari daraja la tatu na utumiaji mdogo wa bima za nyumba.

"Kuanzishwa kwa Bancassurance ilikuwa ni hatua ya kuongeza upatikanaji wa matumizi ya huduma za kifedha, hadi vijijini kwa kutumia mtandao wa matawi ya benki ya msingi wa wateja," alisema Dk. Kibesse.

"Umuhimu wa huduma za bima uko wazi katika maisha ya kila siku ya mwananchi, lakini wanaweza kununua huduma hizo kwa urahisi wanapoelimishwa na wanapofahamishwa. Hakuna raia ambaye hathamini umuhimu wa bima ya afya, sawa na wamiliki wa magari, bima ya maisha, vizuri kupunguza vizuizi vya umma kupata huduma ya bima," alisema Dk. Kibesse. Mwenyekiti wa chuo hicho, Dk. Baghayo Saqware, alisema chuo kina lenga kuweka mazingira sawa yenye ushirikishwaji na ubadilishanaji uzoefu kutoka maeneo tofauti duniani, na kupata wataalamu wa bima ambao watatoa huduma tofauti katika jamii ikiwamo tafsiri za sera zilizo katika lugha ya Kiingereza kuwa Kiswahili.

Alisema, chuo hicho kimelenga kutoa fursa na kuandaa mikutano na kuwataarifu watunga sera kuhusu soko lilivyo pamoja na kukuza vipaji vya vijana barani Afrika kwenye sekta ya fedha.

"Mafunzo haya yamekuja wakati mwafaka kuliko mwingine, taasisi za kifedha ambao zinajishughulisha na Bancassurance zijikite zaidi katika kuwapa mafunzo wafanyakazi wao hasa kuhusu fani hii ya kipekee," alisema Dk. Saqware.

Jumla ya wahitimu 33 walitunukiwa vyeti na naibu gavana waliohitimu kozi ya uwakala wa bima, kilimo na Bancassurance ambazo hutumika kwa ajili ya bima za kibenki.




Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga (mwenye suti), akikabidhi kompyuta na printa kwa wahitimu wanne kati ya 30 wenye miaka 15 hadi 28 waliohitimu fani mbalimbali katika Chuo cha ufundi Mwakata, waliosomeshwa na Shirika la FHI360 kwa ufadhili wa PEPFAR na USAID, ili kuondokana na changamoto ya mitaji baada ya kuhitimu masomo yao jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Watumishi waagizwa kupunguza vikwazo kwa wawekezaji

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imewagiza wataalamu wa sekta zilizo chini ya Wizara ya Uwekezaji kikiwamo Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kupunguza vikwazo kwa wawekezaji nchini ili wavutiwe kuwekeza kwa ajili ya kuongeza mapato ya serikali.

Agizo hilo limetolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geoffrey Mwambe, mjini Morogoro alipozungumza katika kikao kazi kilichowakutanisha wataalamu wa mifumo na wadau mbalimbali katika sekta ya uwekezaji na zile mtambuka kutoka wizara nyingine zenye kushughulika na uwekezaji na biashara.

Waziri Mwambe alisema mfumo huo utamwezesha mwekezaji kukamilisha taratibu zote kwa muda wa siku moja ama tatu ili kuendelea na utaratibu wake mwingine wa uwekezaji ana kuazisha biashara.

Alizitaka mamlaka na taasisi zinazoshughulikia wawekezaji kuweka mfumo mzuri ili kupunguza msururu katika upatikanaji wa leseni kwa wawekezaji hao.

Aliwaonya watumishi wa umma wanapokea rushwa kutoka kwa wawekezaji, hali inayotajwa kurudisha nyuma maendeleo katika sekta hiyo na kwamba watakaobainika wanachukuliwa hatua za kisheria.

Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Dk. Maduhu Kazi, alisema licha ya kuwa na dirisha moja ya huduma kwa wawekezaji, lakini wawekezaji kwa sasa wanalazimika kujaza fomu mbalimbali za kuwezesha kusajili, kupata kibali za kuanzisha biashara ama uwekezaji, kuruhusiwa kufanya kazi na cha mazingira pamoja na vingine wenye kuhusiana na masuakla ya biashara na uwekezaji.

Alisema kikao kazi hicho kinashirikisha wataalamu wa mifumo ya kuwezesha uwekezaji na ufanyaji wa biashara.

Wataalamu kutoka baadhi ya mamlaka na taasisi zinazoshughulika na uwekezaji walitoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Wakala ya Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Idara ya Uhamiaji, Idara ya Kazi, Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA) , Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) na Ofisi ya Waziri Mkuu.

# Kigogo wa halmashauri ahukumiwa kwa rushwa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita imemhukumu Kaimu Mkuu wa Idara ya Maji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Mhandisi Rael Buliba (38), kutumikia kifungo cha miaka 3 jela au kulipa faini ya Sh. milioni 2 kwa makosa mawili ya kupokea rushwa ya Sh. milioni 75.

Alipatikana na hatia ya kupokea rushwa hiyo kupitia kwenye akaunti ya mzazi mwenzake, Edes Joseph, kutoka kwa mkandarasi Francis Nyenge ili apate kuongezewa muda wa mkataba wa kusambaza mabomba ya maji katika mradi huo.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samuel Maweda, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha makosa yote mawili pasipokuacha shaka yoyote.

Hakimu Maweda alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili liwe fundisho kwake na kwa watumishi wengine wenye tabia ya kupokea rushwa.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili Kiongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Kelvin Murusuri, alipeleka hapo mahakamani mashahidi 5 na vielelezo 6, ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda makosa hayo.

Aidha, Hakimu Maweda alisema amelipitia ushahidi wa pande zote mbili na kugundua kuwa upande wa mashtaka umethibitisha makosa yote mawili pasipo kuacha shaka yoyote, hivyo mahakama inamtia hatiani mshtakiwa kwa makosa yote mawili.

Mshtakiwa huyo alipopewa nafasi ya kujitetea, aliiomba aachiwe huru kwa sababu ana familia inayomtegemea.

Hakimu Maweda alitupilia mbali utetezi huo na kusema kuwa makosa ya namna hii ya kuhujumu serikali yamezidi sana, kwa sababu mshtakiwa huyu ni mtumishi wa serikali, na kwamba chakushangaza anaihujumu serikali iliyomwajiri.

Aidha, Hakimu Maweda alisema mahakama inakuhukumu mshtakiwa kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela au kulipa faini ya Sh. milioni moja na kosa la pili mshtakiwa utakwenda jela miaka mitatu au kulipa faini ya Sh. milioni moja. Mshtakiwa huyo alilipa faini ya Sh. milioni mbili kwa makosa yote mawili na kuachiwa huru. Mshtakiwa huyo alikuwa akitetewa na Wakili wa Kujitegemea, Penina Mashimba na upande wa Jamhuri ulikuwa ukiongozwa na Wakili Kiongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Kelvin Murusuri pamoja na Wakili wa Serikali, Daniel Masambu.

Mshtakiwa huyo na wengine wawili walikuwa wakikabiliwa na makosa tisa ya uhujumu uchumi na rushwa ya Sh. milioni 75 za mradi wa maji wa vijiji viwili ambavyo ni Chikobe na Nyamtukuza.

Awali washtakiwa Edes Joseph na Frasinci Nyenge walikiri makosa yao yote na kuhukumiwa kwenda jela miaka minne au kulipa faini ya Sh. milioni 75 na kwa pamoja walilipa faini na kuachiwa huru.

Katika hati ya mashtaka, ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo na wenzake wawili walitenda makosa hayo Machi na Oktoba mwaka 2014, kwa kupokea rushwa ya Sh. milioni 75 kupitia kwenye akaunti ya mzazi mwenzake, Edes Joseph kutoka kwa mkandarasi, Frasinci Nyenge ili apate kuongezewa muda wa mkataba wa kusambaza mabomba ya maji katika mradi huo.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## OMBI LA KUONYESHA NIA: UTOAJI WA HUDUMA ZA URITHI WA KITAMADUNI NA AKIOLOJIA KATIKA UTEKELEZAJI WA MRADI WA UJENZI.
## KUMBUKUMBU NA:10007254

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi,TotalEnergies East Africa Midstream B.V Tanzania, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma Za Urithi wa Kitamaduni na Akiolojia katika utekelezaji wa Ujezi wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la mafuta ghafi litakalofukiwa chini ya ardhi, kuanzia Ziwa Albert nchini Uganda na kuvuka mpaka hadi Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni takriban kilomita 1,443; na kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania. Bomba hilo litapita kwenye mikoa nane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; na pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MPANGO KAZI WA UTOAJI HUDUMA:**

Kampuni ya EACOP imezingatia Hatua Mahususi za Mradi, kufanya utafiti wa kiakiolojia na kijiolojia, juu na chini ya ardhi, katika eneo la Mradi wa bomba la mafuta, na inaendelea kufanya uchunguzi wa kiakiolojia katika maeneo hayo ili kuandaa maeneo ya kipaumbele kwa ajili ya ujenzi wa kambi za wafanyakazi na hifadhi ya mabomba (MCPY) kwa siku zijazo. Mradi unatafuta taasisi ya kitanzania yenye weledi na uzoefu na pia uwezo wa kutekeleza kazi za kiakiolojia wakati wa:

**1.** Kazi za awali za maandalizi na ujenzi wa makambi mbalimbali,

**2.** Ujenzi wa bomba la mafuta ghafi na majengo mengine, pamoja na kuchimba na kuchenjua udongo katika maeneo ambayo hayajapimwa ili kubaini uwepo wa vitu vya kiakiolojia yaliyomo ndani yake. Kazi zote za ujenzi zitatekelezwa kwa kufuata sheria za Tanzania, na viwango vya ufadhili wa kimataifa (International Financing Standards -IFS), zinazoelekeza namna ya kusimamia mambo ya urithi wa kitamaduni na kiakiolojia.

Kazi hii inahitaji mwanaakiolojia mwenye ujuzi na uzoefu mkubwa na mwenye zana na vifaa vyote muhimu vya kazi ili kutoa huduma bora za urithi wa kitamaduni na kiakolojia kwa wakati mmoja katika maeneo mbalmbali, kwa kuwahusisha wadau wa Mradi na Serikali (mfano Idara ya Malikale) kama inavyotakiwa. Huduma za Urithi wa Kitamaduni na Kiakolojia zinajumuisha uchimbaji na uchenjuaji udongo, utambuzi, kutoa muongozo juu ya usimamizi wa muongozo kuhusu hatua Mahususi za Mradi zinazoonyesha nini kitatokea katika malikale zisizotambulika, mafunzo na uhamasishaji, kuandaa nyaraka na kukamilisha kazi ya kufukua masalia katika maeneo muhimu yaliyoainishwa, ufuatiliaji, uhakiki na utoaji taarifa kwa kufuata sheria za Tanzania, viwango vya ufadhili wa kimataifa (International Financing Standards -IFS), na vigezo vya Urithi wa Kitamaduni na Kiakolojia. Kazi itahitaji kuhusisha jamii kuhusu Malikale Zinazoonekana na Zisizoonekana. Utoaji wa huduma za Urithi wa Kitamaduni na Kiakiolojia unahitaji rasilimali, na pia unaweza kuhitaji uratibu wa kazi ya kuchambua na kuhifadhi malikale, kuandaa ripoti na mikutano.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**

Taasisi zinazotaka kuwasilisha nia zao zinaalikwa kuandika maombi yao, na kuambatanisha:

- Sifa na vyeti vya utoaji wa huduma za urithi wa kitamaduni na kiakiolijia.
- Historia fupi ya wataalamu uwa toaji wa huduma za urithi wa kitamaduni na akiolijia.
- Mifano ya uzoefu mahsusi ndani ya miaka 10 iliyopita.

**Uzoefu katika:**

- Kutoa huduma za usimamizi wa urithi wa kitamaduni na kiakiolojia..
- Ufukuaji wa masalia ya malikale ardhini.
- Uzoefu wa kazi za ujenzi na usimamizi wa muongozo kuhusu Hatua Mahususi za Mradi zinazoonyesha nini kitatokea katika malikale zisizotambulika.
- Kuandaa makabrasha na kutoa mafunzo juu ya Urithi wa utamaduni na akiolojia.
- Kufuata Kanuni na Maudhui ya Ndani, ya mwaka 2017, na sheria zinazoongoza taasisi za ndani.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za Mradi.

**Mpango wa kazi huu unaweza kugawanywa kimkoa au kiutalaam na KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja, kadhaa au vyote.**

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kutuma nia zao, pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (barua pepe isizidi 20 Mb), saa **9.00** kamili alasiri au kabla, kwa saa za Afrika Mashariki (EAT), ifikapo tarehe **6 Desemba 2021.** Kichwa cha barua pepe kiwe10007254.

**Angalizo:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazowasilisha nia zao ili kupendekeza na kutengeneza orodha ya taasisi zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndizo zitakazopokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni ili kuingia katika hatua inayofuata ya mchakato wa zabuni. Maombi yote ya kuonyesha nia ya utoaji huduma yanapaswa kuandikwa kwa lugha fasaha ya Kiingereza.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## OMBI LA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA ZA KIBENKI NCHINI TANZANIA
## KUMBUKUMBU NA: 10007186

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V. inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma za kibenki katika mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

Kampuni inahitaji kufungua akaunti za benki katika benki mbili za nchini Tanzania. Akaunti zitatumika kwa matumizi ya malipo ya ndani peke yake kupitia mfumo wa kuhamisha fedha kielectroniki. Malipo yatafanyika katika fedha za Kimarekani (USD) na Shilingi za kitanzania (TZS), kwa watoa huduma wengine, mamlaka za ndani pamoja na waajiriwa.

Huduma hizi hazijumuishi malipo ya nje ya mipaka ya Nchi, fedha ngumu kwa ajili ya matumizi ya dharura (Petty cash), kutoa fedha kuzidi kiwango kilichomo, mkopo, kuweka fedha, na maswala mengine ya kifedha.

Pamoja na orodha ya gharama zitakazowasilishwa na benki, watoa huduma wa ndani ndio watakaohitajika, idadi ya matawi, ushindani kwenye kubadili fedha za kigeni, usaidizi wa maswala ya kiuchumi, usaidizi katika huduma, muda wa kikomo wa siku na muda wa kukamilisha mchakato wa kazi, uwezo wa kuhudumu ndani ya tarahe iliyoombwa kwa ajili ya kufanya malipo pamoja na nafasi ya benki katika soko. Na pia utayari wa benki kushiriki katika kuwekeza fedha katika deni la nje linalotarajiwa la kibiashara.

**VIGEZO MUHIMU:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Uthibitisho wa Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa katika mawanda ya kazi.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Inashauriwa, muoneesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao kwa lugha ya kiingereza pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacoptz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **2nd Desemba 2021.** Kichwa cha Habari cha barua pepe kiwe ni kumbukumbu namba husika tu. Kichwa cha Barua Pepe kiwe ni **10007186.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jicho, maombi yetu kwa Simba kulinda nafasi 4 michuano CAF

**PAMOJA** na kuingiza timu nne msimu huu kwenye michuano ya kimataifa ngazi ya klabu inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF); mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho, hatimaye Tanzania imebaki na mwakilishi mmoja tu, Simba katika mashindano hayo yanayoongoza kwa utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu Afrika.

Hiyo ni baada ya Azam FC na Biashara United zilizokuwa zikiiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho baada ya Yanga kuwa ya kwanza kuaga katika Ligi ya Mabingwa kwa kutolewa raundi ya awali na Rivers United ya Nigeria.

Pengine Biashara United ingeweza kuwa mashindanoni kutokana na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya iliyoupata katika mchezo wa awali Uwanja wa Benjamin Mkapa, lakini ilishindwa kwenda kwenye mechi ya marudiano ugenini kutokana na changamoto ya vibali vya kutumia anga ya Sudan, Sudan Kusini na Libya, hivyo CAF ikaiondoa kuwapa Walibya hao nafasi ya kusonga mbele.

Hivyo kuifanya Tanzania kubaki na timu moja, Simba ambayo nayo ilitolewa na Jwaneng Galaxy ya Botswana kwenye raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kuangukia Kombe la Shirikisho ambapo sasa itacheza mechi moja nyumbani na ugenini dhidi ya Red Arrows ya Zambia na kama ikipata matokeo ya jumla itatinga hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Kwa maana hiyo, matarajio pekee kwa Tanzania katika kutetea kuingiza tena timu nne msimu ujao kwenye michuano hiyo ya CAF, ipo mikononi mwa Simba.

Kibarua cha kwanza cha Simba katika kusaka nafasi ya kucheza hatua ya makundi, kitakuwa Jumapili wiki hii itakapoikaribisha Red Arrows katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kabla ya kurudiana nchini Zambia Desemba 5, mwaka huu.

Kikubwa kwa sasa ni Simba kujiandaa vema kuelekea mchezo huo ili kuhakikisha inapata ushindi wa kishindo nyumbani kabla ya kwenda kumaliza kazi ugenini, huku ikitambua Watanzania wote wapo nyuma yao wakitaka kuona inapigania kulinda nafasi hizo nne. Ikumbukwe hadi sasa tayari Libya imefikisha pointi za kuingiza timu nne kwenye michuano ya CAF msimu ujao, hivyo kama Simba ikishindwa kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho na kufanya vizuri kwenye michuano hiyo, ni wazi Tanzania itarudi kwenye timu mbili; moja Kombe la Shirikisho na nyingine Ligi ya Mabingwa kwa msimu ujao.

Hivyo, huu ni wakati ambao Watanzania wanapaswa kuwa kitu kimoja kwa kuanza kuiombea Simba katika maandalizi yake hadi siku itakapocheza mechi hizo mbili nyumbani na ugenini kwa kila mmoja kutambua kwamba inalipigania taifa katika kutetea nafasi hizo nne. Huu si wakati wakutanguliza mbele itikadi zetu za 'kiklabu', lakini ni kipindi ambacho mashabiki wote wa soka wanapaswa kuweka kando tofauti zao na kuwa kitu kimoja katika kuiombea na kuitakia mema Simba isonge mbele kwenye michuano hiyo.

Nipashe tukiwa wadau namba moja wa michezo nchini, tunatambua wazi ili kuwa na matarajio makubwa ya timu zetu kufanya vizuri hatuna budi kupigania kuingiza klabu nne kwenye michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Tunaamini kwa yeyote asiyeipa Simba sapoti katika michuano hiyo kwa sasa, ni sawa na kutokukubali Tanzania kupata nafasi nne katika michuano hiyo msimu ujao jambo ambalo halina tofauti na kuihujumu nchi kisoka.

Lakini, pamoja na maandalizi makubwa ambayo tunaamini Simba inayafanya kuelekea mchezo huo, mashabiki na Watanzania kwa ujumla hatuna budi kujitokeza kwa wingi Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili ili kuipa sapoti wakati ikicheza dhidi ya Red Arrows.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Marefa sasa watafukuza watazamaji Ligi Kuu Bara

**HAIKUWA** kazi rahisi kuwashawishi Watanzania kuangalia mechi za Ligi Kuu na kuacha Ligi ya England, au kulazimika kuangalia kwa pamoja.

Ni kazi ngumu iliyofanyika kuwashawishi na kwa sasa Ligi ya Tanzania ni moja kati ya ligi zinazoangaliwa na watu wengi si hapa tu, bali ukanda wote huu wa Afrika Mashariki na Kati hadi Kusini.

Ni watu waliamua kuacha kazi na kufanya kazi, kuna watu waliwashawishi mashabiki kwa kuwekeza kwenye soka, yapo makampuni mengi yameanza kujitokeza kudhamini klabu pamoja na soka lenyewe kwa ujumla kupitia Shirikisho la Soka nchini (TFF).

Wapo watu binafsi ambao nao baada ya kuona soka limeanza kuwa na mvuto kwa mashabiki, wamewekeza kwenye klabu walitoa pesa nyingi, si kwa ajili ya wao kupata faida, bali kuufanya mchezo wa soka kuendelea kuwa kituvio, lakini kuendelea kutengeneza vijana kwa ajili ya timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars.

Wakati TFF, makampuni, na wadau wakilifanya soka la Tanzania kung'ara ndani na nje ya mipaka ya nchi, kumeanza kutokea mambo ya ajabu yanayotaka kurudisha soka la Tanzania kwenye zama za giza. Si wengine ni baadhi ya waamuzi.

Waamuzi ni moja kati ya watu ambao wanafanya soka la nchi liendelee, kuwa na ligi bora au mbovu, pia kutoa mwakilishi bora kwenye mechi za kimataifa, kutoa mwakilishi dhaifu na feki. Pamoja na kwamba Ligi Kuu ya Tanzania imeanza kwa mvuto, kuwa ngumu kutokana na kila timu kuonekana kujipanga kisawasawa, huku zikichagizwa na pesa zilizowekwa na wadhamini Azam Media, pamoja na NBC, baadhi ya waamuzi wameonekana kuanza kuharibu mapema kabisa.

Hata mzunguko wa kwanza haujafika kumekuwa na matukio mengi ambayo waamuzi wametoa maamuzi yasiyo sahihi na kuzipokonya timu ushindi au sare.

Tuliona mechi ya Yanga dhidi ya Azam, Idd Nado akikwatuliwa ndani eneo la hatari, lakini mwamuzi kwa sababu zake alishindwa kutoa penalti. Fiston Mayele alizawadiwa penalti baada ya yeye mwenyewe kushika mpira.

Mbaraka Yusuph alifunga bao la kuotea dhahiri, akiisawazishia Kagera Sugar, ingawa kwa bahati Geita Gold ikapata bao la pili baadaye na timu yake kulala kwa mabao 2-1. Kali kuliko yote, mwamuzi Abel William kutoa mkwaju wa penalti kwa Yanga, baada ya Feisal Salum kunyang'anywa mpira kirahisi ndani ya 18.

Ukilirudia tukio lile hata mara 100, hakuna hata dalili za kusema ilipashwa kuwa penalti. Mchezaji aligusa mpira na Fei Toto alianguka mwenyewe.

Ukishangaa ya Mussa utaona ya Firauni, sasa hata hiyo penalti yenyewe ilivyopigwa hata mechi za mchangani haiwi vile. Ni aibu kubwa kwa soka la Tanzania ambalo linatazamwa hata nje ya mipaka yetu.

Wakati Saido Ntibazonkiza anapiga penati hiyo, jumla ya wachezaji watano wa timu zote mbili walikuwa wameingia ndani ya dimba. Fei Toto alionekana kuingia kiasi cha kutaka kumpita mpigaji na bado likaruhusiwa kuwa ni bao, badala ya kurudiwa. Ni tukio lililoleta vurugu hata kwenye vibanda umiza. Kuna baadhi ya mashabiki kwenye kibanda umiza walianza kuondoka, wengine waliongea maneno makali, ilibaki kidogo hata mwenye kibanda apigwe. Wengine wakitamka kabisa kuwa bora kuangalia mpira wa Ulaya ambao hauna makandokando, lakini si huu wa Tanzania. Unaanza kujiuliza kama hawa watu wangekuwa uwanjani sijui ingekuwaje?

Ni kweli kuna baadhi ya matukio hata waamuzi wa nje wanasaidiwa wa VAR, lakini kuna mengine waamuzi wanakuwa hapo hapo, ila wanababaika kutoa maamuzi yasiyo sahihi. Unajiuliza kama sheria za soka huwa zinabadilika kutokana na timu inayocheza au zinafanya kazi kwa wote.

Inafikirisha mwamuzi aliyekataa kutoa penalti kwenye mechi ya Simba dhidi ya Ruvu Shooting baada ya Bernard Morrison kukatwa ndani ya eneo la hatari, na yule aliyetoa penalti kwa beki kumnyang'anya Fei Toto mpira. Makocha, wachezaji, wadhamini na wafadhili wanafanya kazi kubwa ili kuufanya mpira kuwa na thamani, lakini unaonekana kuharibiwa na baadhi ya waamuzi kwa sababu wanaozijua wao wenyewe.

Ifike wakati sasa TFF, Bodi ya Ligi (TPLB) na Chama cha Waamuzi (FRAT) kilinde thamani ya ligi yetu kwa kuwapa adhabu kali waamuzi wenye tabia hii ili iwe fundisho kwa wengine. Isipochukua hatua kesho na keshokutwa tunaweza kushuhudia vituko vingine zaidi ya hivi tunavyoanza kuvishuhudia ligi ikiwa ndiyo kwanza bado asubuhi.

Na mashabiki hawatoiamini tena na kuanza kukimbia ndiyo watu waanze kutafuta nini chanzo cha kupungua mashabiki viwanjani na kwenye kibanda umiza wakati 'mchawi' anajulikana. Waamuzi waache kutengeneza matokeo, kwa sababu hapa anatafutwa mwakilishi wa nchi. Apatikane kwa uwezo wake ili akaiwakilishe nchi vizuri na si wa kuchongwa, matokeo yake mechi za kwanza tu tunatolewa, huku kila mtu na wachambuzi wakitoa sababu nyingi ambazo hazipo.

Kumbe nchi ilikuwa na mwakilishi feki, na huko hakuna kubebana. TFF ichukue hatua kali kwa waamuzi hawa kwa ajili ya kulilinda thamani ya soka la Tanzania.

# Mchengerwa aipa TAKUKURU wiki mbili upotevu madini Mererani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti na Utumishi wa Umma), Mohamed Mchengerwa, ametoa wiki mbili kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU), kufuatilia wizi wa madini katika mgodi wa serikali wa Mererani ulioko mkoani Arusha.

Kadhalika, ameagiza taasisi hiyo pia kuchunguza ubadhirifu wa fedha za umma katika Chuo

Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa mfumo wa ajira kiganjani Ajira Poto mobile APP, alisema kumekuwa na maneno kila kona kuhusiana na wizi wa madini

mkoani Manyara na Arusha ambao unalitia hasara taifa, na kwamba ni vyema TAKUKURU wakachunguza.

"Nawapatia wiki mbili kuhakikisha mnafanya uchunguzi wa kina ili kubaini wezi wa madini hayo, tunahitaji kuona taifa linakuwa kiuchumi na si kusikia wezi wanaorudisha maendeleo nyuma," alisema Mchengerwa.

Alisema taasisi hiyo inapaswa kuingia kazini kuhakikisha wezi hao wanabainika kabla ya kuendelea kuharibu mali ya serikali bila kibali chochote.

Aidha, aliwataka TAKUKURU kutumia utaalamu wao kuhakikisha madini ya serikali yanakuwa salama na siyo kuchezewa na watu.

Pia, aliwaagiza wakuu wa wilaya na mikoa kuhakikisha fedha za miradi zinazotolewa na serikali zinatumika kuleta matokeo chanya na siyo kuchezewa na ovyo.

Waziri Mchengerwa aliwataka wakuu hao kuhakikisha fedha zinapofika moja kwa moja zinakwenda kufanya kazi ya kuendeleza miradi ya serikali maeneo yote.

"Enyi wakuu mlioteuliwa na Rais hakikisheni mnakwenda kufanya kazi ya miradi iliotukuka na sio kuachia fedha za miradi zinapotea bila sababu yoyote,"alisema waziri huyo.

Kuhusu fedha za UDOM, aliitaka TAKUKURU kufuatilia na kubaini wahalifu wanaofanya mambo hayo kukidhalilisha chuo hiko, na kwamba atahitaji taarifa ya kina itakayokuwa na majibu sahihi ya upotevu huo.

Kuhusu mfumo aliozindua wa Ajira Poto ambazo unazipata katika simu ya kiganjani, alisema itapunguza changamoto kwa waombaji ajira. Naye Naibu Waziri, Deo Ndejembi, alisema Ajira Poto itawawezesha vijana wengi kuona matangazo ya ajira ikiwamo kuomba kutokana na kwamba kila kitu kitakuwa wazi katika simu hizo.




Meneja wa NMB Tawi la Msasani, Kelvin Mwangosi, akibonyeza kitufe cha kompyuta kumtafuta mshindi wa droo ya sita ya msimu wa pili wa Kampeni ya Weka Akiba na Ushinde inayoendeshwa na Benki ya NMB "Bonge la Mpango – 2merudi Tena", iliyochezeshwa kwenye tawi la benki hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto anayeshuhudia ni Msimamizi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Neema Tatock na kulia ni Ofisa Huduma kwa Wateja wa benki hiyo, Neema Kazoviyo. **PICHA: NA MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima washauriwa mbegu za muda mfupi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKULIMA wilayani Njombe wameshauriwa kupanda mbegu za mazao ya muda mfupi, ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Ofisa Kilimo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Lwimiko Mellah, aliyasema hayo hivi karibuni wakati wa uzinduzi wa ugawaji wa pembejeo wa Shirika lisilo la kiserikali la One Acre Fund uliofanyika kijiji cha Matembwe.

Alisema Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imeshatangaza kuwa mvua itanyesha chini ya wastani, na ndiyo maana wanawaelimisha wakulima ili wasipate hasara.

"Sasa mvua zinaponyesha chini ya wastani sisi maofisa ugani tunasisitiza wakulima watumie mbegu zinazostawi. Zinazostawi kwa muda mfupi au zinazozaa kwa muda mfupi sambamba na kustamili mabadiliko ya hali ya hewa zile mvua chache zinazoendelea kunyesha," alisema Mellah.

Pia, alisema wanaendelea na zoezi la kutoa elimu kwa wakulima pamoja na kwamba mbolea ya DAP kuwa na bei kubwa, lakini kuna mbadala kama NPS.

Naye Ofisa Uhusiano wa serikali kutoka Shirika la One Acre Fund, Neema John, alisema progamu hiyo ilianzishwa ili kuwapa wakulima upatikanaji wa bidhaa zinazoboresha maisha yao kwa kupeleka pembejeo za kilimo kwa vijiji vya mbali karibu na wakulima ili kubadilisha maisha yao. "Programu yetu inatoa fursa kwa wakulima kuchukua pembejeo kwa mkopo na kufanya malipo kidogo kidogo kwa kipindi cha msimu mzima, kutokana na bei ya mbolea kuwa juu tumepunguza ada yetu ya mkopo kutoka asilimia 19 hadi asilimia 10 na hatutozi gharama za usafiri bali tunamfikishia mkulima hadi kijijini," alisema Neema.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, amepongeza mpango huo wa kukopesha wakulima mbolea kwa kuwa utasaidia kuendeleza shughuli za kilimo. "Tunatamani wadau wengine waige mfano huu wa One Acre Fund ili kuwasaidia wakulima wetu kuendelea kupata tija, serikali inafanya kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na ndiyo maana leo hii taasisi inagawa pembejeo, lakini serikali ipo," alisema Kasongwa. Mmoja wa wakulima waliopata mkopo huo, Evalist Msimike, alisema kukopeshwa mbolea ni nafuu kwao kwa sababu sasa wana uhakika wa kuendesha shughuli zao za kilimo bila ya kuwaza suala la mbolea.

# Jiji Dar laagiza choo bora kila kaya

**Na Christina Mwakangale**

UONGOZI wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, umewaagiza viongozi wa mitaa, ikiwamo watendaji na wenyeviti wa mitaa, kata, kuhakikisha kila kaya ina choo bora ili kuepukana na magonjwa ya mlipuko.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu, Ludigija, amesema ni muhimu hadhi ya Jiji la Dar es Salaam, iendane na makazi pamoja na maeneo ya biashara yenye vyoo bora.

Ludigoja alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati akipokea vifaa vya kufanyia usafi kutoka Shirika la WaterAid, vyenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa ajili ya Kituo cha Afya ya Mama na Mtoto Chanika-Nguvu Kazi pamoja na Buguruni, kuadhimisha Siku ya Choo Duniani.

Alilipongeza Jiji hilo kwa kushirikiana na wadau kupitia kampeni ya usafi wa mazingira kutoka asilimia 70 hadi 95.4 ya malengo, na kwamba asilimia iliyobaki ifikiwe ili mji uwe safi na kuepuka na maradhi ya mlipuko.

"Zamani tulishuhudia maradhi ya mlipuko kama kipindupindu kutokana na utiririshaji maji machafu. Ndio maana yalijengwa mabwawa maji ya kutunza maji machafu kwenye baadhi ya maeneo kulikokithiri magonjwa.

"Kwa miaka mitano hatujashuhudia magonjwa ya mlipuko. Tutahakikisha kila kaya ina vyoo bora. Ujenzi wa kila nyumba uzingatie uwepo wa choo kuendana na hadhi ya jiji," alisema Ludigija. Mkurugenzi Mkazi wa Wateraid, Anna Mzinga, katika taarifa yake kusuhu siku hiyo inayoadhimishwa kila Novemba 19, alisema wanaungana na taasisi nyingine kwenye maadhimisho ya mwaka huu yenye kauli mbiu Kipe Hadhi Choo Chako.

Anna alisema vifaa hivyo ni mafagio, sabuni, mikokoteni, mabuti, majaketi ang'avu, glavu ngumu kushirikiana na wadau kufanya usafi katika hospitali hizo, shule za msingi nane zilizopo katika wilaya ya Ilala.

"Napenda kuipongeza serikali kwa juhudi kubwa ambayo imefanya mpaka hivi sasa, kwa mujibu ya ripoti ya Wizara ya Maji, kwa mwaka jana mafanikio yanaonyesha asilimia 66 ya kaya Tanzania wana vyoo bora majumbani ukilinganisha na asilimia 31 mwaka 2016."

Ofisa Afya wa Jiji la Dar es Salaam, Reginald Mlay, alisema kampeni ya usafi jiji, tangu ilipoanza mwaka 2012 imefanyika kwenye kata 36 na mitaa 159, ambayo imepunguza kiwango cha maradhi makazi ya watu.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Chanika-Nguvu Kazi, Dk. Paschal Nkii, alimwomba Mkuu wa Wilaya kwa kushirikiana na wadau kufanikisha upatikanaji wa majisafi kutoka DAWASA, kutokana na maji wanayotumia hospitalini hapo hivi sasa kuwa na kiwango kikubwa cha chumvi.

# NEMC yaonya uharibifu vyanzo vya maji

**Na Maulid Mmbaga**

BARAZA la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), limekiri kukithiriwa kwa uharibifu wa mazingira nchini huku likisisitiza kuendelea kuwachukulia hatua za kisheria kwa watakaobainika kuharibu vyanzo vya maji.

Aidha, limezitaka bodi za mazingira katika vijiji, wilaya na mikoa kutimiza wajibu wao.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam Mkurugenzi Mkuu (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, alisema uharibifu wa mazingira umekithiri kutokana na watu kutozingatia sheria na sera za mazingira kwa kuharibu vyanzo vya maji na uoto wa asili.

Alisema agizo la Rais Samia Suluhu Hassan alilolitoa kwa wakuu wa mikoa kuhusu ulinzi wa vyanzo vya maji linapaswa kuzingatiwa ili kuhakikisha kuwa ustawi wa maji unaendelea kuwapo nchini.

"Hakuna asiyejua hali halisi tuliyonayo sasa hivi, lakini pamoja na mabadiliko ya tabianchi, sehemu kubwa zaidi ya upungufu wa maji imechangiwa na shughuli za kibinadamu, hivyo sisi kama baraza ni wajibu wetu kushirikiana na wakuu wa mikoa kulinda vyanzo vya maji.

"Vyanzo vya maji ni sehemu ya mazingira ambayo yanasimamiwa na sheria ya mazingira ya mwaka 2004, na moja ya majukumu yetu ni kutoa elimu kwa jamii kwani uharibifu mkubwa unaotokea kwenye vyanzo vya maji unatokana na wananchi kukosa elimu," alisema Dk. Gwamaka.

Aliongeza kuwa katika maeneo mengi nchini kuna mmomonyoko wa ardhi na makorongo kwa sababu sehemu kubwa uoto asili umeharibiwa na shuhuli za kibinadamu, na alibainisha kwamba maeneo oevu yamepungua nchini akitolea mfano bonde la Ihefu.

Dk. Gwamaka alibainisha kuwa sehemu nyingi oevu zimevamiwa kwa watu kujenga makazi na kuendesha shuhuli za kilimo, na kusababisha uhifadhi wa maji ardhini kupungua.

Aidha, alisema kuwa kutotekelezwa kwa sheria ya mazingira, ambayo inatoa mamlaka kwa serikali kuanzia ngazi ya mkoa, wilaya, vijiji na vitongoji kusimamia mazingira kwenye maeneo yao.

"Kamati hizi hazifanyi kazi na matokeo yake unakuta kwamba maeneo mengi ambayo yalipaswa kuachwa yale oevu yanayoendelea kutunza maji kwa mwaka mzima yamevamiwa, sina haja ya kutaja mifano, lakini hiyo imesababisha chemchemu nyingi kukauka.

"Sasa hivi kumekuwa na tabia watu kuanzisha miji hovyo hata katika maeneo oevu ambayo niya asili yanayotakiwa kuachwa ili yaendelee kutunza maji, sheria ipo inazungumza wazi kabla hujaanza kujenga mji lazima ufanye tathimini ya kimkakati ya mazingira, lakini miji inaanzishwa pasi na kufanya tathmini," alisema Dk. Gwamaka.

Alieleza kuwa kutokana na hilo, inatafsiri kwamba mamlaka za serikali za mitaa zimedharau sheria ya mazingira ya mwaka 2004, kwa kuanzisha na kupitisha masuala hayo bila kufanya tathmini jambo linalosababisha kutokea kwa uharibifu mkubwa wa mazingira.

Dk. Gwamaka alisema kuwa makorongo yamekuwa mengi mkoani Dar es Salaam kutokana na kutokuzingatiwa kwa sheria ya mipango miji, aliwataka Watanzania kila mmoja kujitafakari anachokifanya na kujiepusha na shughuli zinazosababisha uharibifu wa vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla.

"Ule mchanga tunaouona Msimbazi si kwamba ulikuja kwa bahati mbaya, kuna watu ambao wameharibu mazingira kwa kukata miti na kuondoa uoto asili unaosaidia katika uhifadhi wa maji ardhini na kusababisha maji kutengeneza makorongo kutokana na uwingi.

"Maji yanapoanza kuporomoa yanazoa mchanga na nyumba ndio matokeo tunayoyaona kule Msimbazi, nitoe rai kwa Watanzania tujifunze kutunza mazingira, isifike mahali hadi Rais atukumbushe wakati ni wajibu wetu, na kamati za mazingira zilizotajwa kisheria zitekeleze majukumu yake," alisema.




Meneja Uhusiano wa Vodacom Tanzania, Alex Bitekeye, akikabidhi tuzo kwa klabu ya Shule ya Sekondari Tambaza baada ya kuibuka washindi wa tatu kwenye hafla ya Uwezo Award Ceremony 2021. Vodacom Tanzania Foundation ilidhamini tuzo hizo zenye lengo la kuwahamasisha wanafunzi kuonyesha vipaji vyao, hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni wa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shaka ashupalia upotevu wa mabilioni ya serikali

**Na Beatrice Shayo,** KIGOMA

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, amewataja wanaohusika na upotevu wa zaidi ya Sh. bilioni 2 kila mwezi katika ukusanyaji wa mapato mkoani Kigoma, wakiwamo wafanyabiashara na baadhi ya watumishi wa serikali.

Shaka aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati alipofanya ziara ya Sekretarieti ya CCM wakifuatilia utekelezaji wa ilani ya chama katika mkoa wa Kigoma walitembelea bandari na reli.

Alisema maeneo hayo ni sehemu ya ukusanyaji wa mapato ya serikali kwa upande wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ingawa bado hawajafanya vizuri, lipo eneo ambalo linalegalega.

"Nikupongeze Meneja mpya wa TRA, Gabriel Mwangosi, umekuja ni matumaini yangu kwamba utaanza na haya, nina taarifa kuwa umeanza vizuri hongera...endelea kusimama vizuri meneja unajua zaidi ya Sh. bilioni 2 kwa mwezi zinapotea kwenye ukusanyaji wa ushuru wa forodha hili halipo sawa,"alisema Shaka.

Alisema mapato yanayokusanywa kwa mwezi kwa sasa ni Sh. milioni 700 fedha hizo zinapotea katikati mjiulize zinakwenda wapi na kwa nini haziingii katika mfuko wa serikali.

"Wapo wafanyabiashara ambao wanajulikana yupo ambaye ni wakati kazi yake ni kuchezesha ili kuona mapato ya katikati yanakwenda kwake na unao wafanyakazi ambao sio waaminifu wanashirikiana kuhujumu mapato ya serikali," alisema Shaka. Aidha, Shaka alisema fedha hizo zikiingia katika mfuko wa serikali itasaidia kuubadilisha mkoa wa Kigoma kiuchumi na kutatua changamoto zinazowakabili.

"Mmenieleza mnachangamoto ya wafanyakazi na magari hii Sh. bilioni mbili inayopotea kwa mwezi ikisimamiwa vizuri mnauwezo wa kuwalipa watumishi na mnanunua magari, lakini sasa inapotea hewani inakwenda mifukoni kwa watu meneja tunakuomba katika hili tunafungua uchumi wa wa Kigoma na ninyi mjipange vizuri," alisema Shaka.

Aliongezea kuwa: "Mimi nina amini kuletwa kwako hapakuwa kwa bahati mbaya tumefuatilia huko ulikotoka ulifanya vizuri na hapa tuna matumaini kwamba utakuja kubadilisha hizi changamoto zilizokuwa katika huu mkoa wa Kigoma sisi kwa miaka mitano tumeahidi kuijenga nchi hii."

Alisema fedha hizo zinazopotea zinaweza kuboresha upatikanaji wa boti ya doria ambayo ingesaidia kufanikisha shughuli za ukusanyaji wa mapato ndani ya ziwa.

Alisema Rais Samia Hassan Suluhu anafanya jitihada kubwa ili kuwatoa walipo waweze kupiga hatua kama baadhi yenu wakiwa ni wakwamishaji hawatakuwa na dhamira njema na nchi.

# Wananchi watakiwa kufanyakazi kwa bidii

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema inaendelea kusisitiza ufanyaji kazi kwa watu wake, kwa kuwa maisha bora yanapatikana kwa kujituma kwa ufanisi zaidi hususani katika uimarishaji maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Akizungumza juzi mkoani Morogoro katika mahafali ya 32 ya Chuo cha Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) Kihonda, Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Janeth Chata, aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, alisema taifa linatambua umuhimu wa kuwapo kwa vyuo vya ufundi stadi nchini katika kusaidia kuwaandaa wataalamu katika nyanja mbalimbali za ufundi.

Chata alisema vyuo hivi ni sehemu muhimu ya kuwaandaa vijana kukabiliana na soko la ajira na vijana kupata ujuzi wa kujiajiri wao wenyewe.

"Nawapongeza wahitimu wote mnaotunukiwa vyeti leo katika fani zenu mbalimbali ni jambo zuri mmelifanya kwa juhudi na azma yenu ya kutafuta ustadi katika fani mlizojifunza,"alisema.

Alisema miongoni mwa fani walizosoma wahitimu hao ni pamoja na mafundi magari, zana za kilimo, umeme wa magari, vyuma na vipuri mbalimbali, hivyo wanapaswa wanapotengeneza magari au vipuri kuhakikishi kuwa mnatengeneza kwa ubora unaotakiwa.

Chata alisema kwa mafundi wa fani za ujenzi, umeme wa majumbani, majokofu na viyoyozi, wakumbuke kuwa kazi zao huwa zinaonekana na kila mtu hivyo kuhakikisha wanafanya kazi kwa ufanisi mzuri na ubora unaotakiwa.

"Wahitimu mnatakiwa kufanya kazi kwa ubora zaidi huko mnapoenda tambueni kuwa mnapofanya kazi vizuri ni sehemu mojawapo ya kujitangaza na kujipatia ajira binafsi kwa urahisi zaidi," alisema.

Mkuu wa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma VETA Kihonda, Kashindye Maganga, alisema chuo chao ni mojawapo ya vyuo vilivyopo nchini ambavyo vipo chini ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).

## HABARI KITAIFA

# Ununuzi vifungashio nje ulivyowaathiri wakulima

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAFANYABIASHARA wa maduka ya pembejeo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mlowo, wilayani Mbozi, mkoani Songwe, wanadaiwa kuwahujumu wakulima kwa kununua mifuko ya vifungashio nchi jirani na kuweka mbegu za kienyeji kwa madai kuwa zimefanyiwa utafiti (mbegu bora) na kuwauzia wakulima.

Kufuatia tabia hiyo ambayo imekuwa ikilalamikiwa na wananchi, Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo Mlowo (TEO), Joel Kaminyoge, akizungumza na wenyeviti wa vitongoji katika kikao cha baraza la mamlaka hiyo, aliwaonya wafanyabiashara wanaofanya hujuma hizi.

Alisema hivi karibuni kumeibuka kundi la wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu, ambao huenda kununua mifuko ya vifungashio katika nchi jirani za Zambia na Malawi kisha kuweka mbegu za kienyeji kwa madai kuwa ni mbegu bora.

"Ndugu wenyeviti pamoja na mji wetu kuendelewa kustawi vizuri, bado tumeendelea kuwa na changamoto mbalimbali za kiusalama, likiwamo hilo la baadhi ya wafanyabiashara kufanya hujuma za kuwauzia pembejeo feki wakulima na kuwasababishia hasara kubwa," alisema.

Aliwataka wenyeviti hao wa vitongoji katika mamlaka hiyo kwenda kufanya uchunguzi kwenye maeneo yao na kuwabaini wale wote wanaofanya hujuma hizo, ili mamlaka zichukue hatua za kisheria.

"Tuna taarifa kuwa shughuli hizi za kufunga mbegu feki za mahindi baada ya wafanyabiashara wasiowaaminifu kuingiza vifungashio toka nchi za Malawi na Zambia huwa zinafanyika katika baadhi ya misitu ya maeneo myayowaongoza na kwenye majumba wanakoishi wananchi wenu," alifafanua.

Aidha, alisema mbali na hujuma hizo, pia kuna kundi la vijana katika mji huo, ambao wameacha kufanya shughuli halali za kujipatia kipato badala yake wamejiingiza kwenye shughuli haramu za kuwa mawakala wa kusafirisha wahamiaji haramu na kuugeuza mji huo kuwa kitovu cha biashara hiyo haramu.

Hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, aliwatahadharisha wakazi wa Mji wa Mlowo, wilayani Mbozi ambao wanajihusisha na biashara ya kusafirisha wahamiaji haramu, ikiwamo wamiliki wa nyumba za kulala wageni, ambazo zinadaiwa kutumika kuwahifadhi kabla ya kusafirishwa kwa bodaboda hadi maeneo ya mipakani.



Mjumbe Maalum wa Waziri Mkuu wa Uingereza, anayeshughulikia masuala ya Biashara kati ya Uingereza na Tanzania, Lord Walney (kulia), akiangalia baadhi ya bidhaa zinazozalishwa na kampuni ya Serengeti Breweries Ltd (SBL), alipofanya ziara ya kikazi kiwanda SBL Moshi, mkoani Kilimanjaro juzi. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni 81 za China zanunua soya nchini

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

KAMPUNI 81 za China zitanunua soya kwa wakulima wa Tanzania baada ya nchi hizi mbili kusaini mikataba ya uuzaji, lengo likiwa kutafuta soko la uhakika kwa wakulima.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi msaidizi wa uendelezaji wa mazao pembejeo na ushirika kutoka Wizara ya Kilimo, Beatus Malema, katika kikao cha tathmini ya mradi wa mahindi unatekelezwa na Chuo Kikuu cha Kilimo cha China.

Alisema hatua ya kusainiwa kwa mikataba hiyo ni jitihada zinazoendelea kufanywa na serikali katika kutafuta masoko ya uhakika kwa wakulima ili kuwainua kiuchumi.

"Baada ya serikali kusaini mikataba na China tayari kampuni 81 za kununua soyo zimejitokeza, na sisi tumeziambia hizo kampuni zije nchini waweze kuingia kilimo cha mkataba na wakulima wetu ili kuwahakikishia masoko zaidi," alisema Malema.

Ernest Mkongo, mratibu wa mradi huo chini ya ufadhili wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha China, alisema mradi wa kilimo cha soya utatekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja wa 2021/2022 ambapo jumla ya vijiji 4 vitahusishwa.

Alivitaja vijiji hivyo ni Kitete, Peapea, ambavyo vipo wilayani Kilosa na kijiji cha Mkono wa Mara ambacho kipo katika Halmashauri ya Morogoro ambapo jumla ya wakulima 24 kutoka katika kila kijiji watafikiwa na mradi huo.

"Mradi huu wa kilimo cha soyo umekuja baada ya wenzetu wa Chuo cha Kikuu cha Kilimo China kuona mafanikio makubwa katika mradi wa kilimo cha mahindi ambapo tumeona kwamba awali mkulima alikuwa anapata gunia 4 hadi tani kwa hekari moja, lakini baada ya mradi wanavuna hadi gunia 20 kwa heka," alisema Mkongo.

Aliongeza kuwa lengo la miradi yote hiyo ni kusaidia kupunguza umaskini kwa wakulima nchini kwa kufanya kilimo chenye tija na endelevu na kuwataka wananchi wanaopitiwa na miradi hiyo kutumia fursa hiyo vizuri.

Mkuu wa Wilaya ya Ulanga, Ngolo Malenya, alikishukuru Chuo Kikuu cha Kilimo cha China kwa kutekeleza mradi huo mkoani Morogoro na kuahidi serikali ya mkoa huo kuendeleza ushirikiano na chuo hicho katika kuwaletea maendeleo wananchi.

## Selcom, NMB zaunganisha nguvu malipo ya kidijitali

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB na kampuni ya Selcom Tanzania zimetangaza kushirikiana kusaidia kupunguza matumizi ya pesa taslimu nchini.

Hatua hiyo iliyofikiwa mwishoni mwa wiki ni kuifanya Tanzania kuwa taifa la uchumi wa kidijitali lenye matumizi madogo ya pesa taslimu.

Akiutaja ushirikiano huo kuwa maendeleo makubwa, Mkuu wa Idara ya Biashara za Kadi wa NMB, Philbert Casmir, alisema benki hiyo imekuwa mstari wa mbele kwenye mapinduzi ya malipo nchini.

Pia alisema ubia huo unawapa wateja wa NMB na Selcom pamoja na wamiliki wa simu za mkononi mawanda mapana zaidi ya sehemu za kufanyia malipo na kuchagua namna ya kulipia bidhaa na huduma mbalimbali.

Kutokana na hatua hiyo, sasa wateja wa NMB wanaweza kuvitumia vituo vya miamala vya Selcom kufanya manunuzi na wamiliki wa simu za mkononi kufanya malipo kupitia mfumo wa msimbo wa NMB (QR Codes) ambao pia utatumiwa na wateja wa Selcom.

Wakati NMB ina zaidi ya sehemu 53,000 kwenye mtandao wake wa mfumo wa malipo wa msimbo, Selcom ina karibu idadi kama hiyo ya vituo vya kufanyia miamala nchini kote.

"Ubia wa kimkakati na ubunifu kama huu ni muhimu katika kufikia ndoto ya kuifanya Tanzania kuwa jamii ambayo imeachana na matumizi ya fedha taslimu, na tutaendelea kujitolea kwa hali na mali kubuni suluhisho za malipo zinazoendana na hali halisi na mahitaji ya soko," alisema Casmir.

Aliongeza kuwa lengo la mama la ushirikiano huo ni kuimarisha huduma jumuishi za kifedha nchini, kujenga mfumo mpana wa malipo, na kuongeza wigo wa suluhisho za malipo za kisasa.

"Tunafurahi kushirikiana na Selcom ili kuimarisha zaidi mfumo jumuishi wa haraka wa kufanya malipo nchini Tanzania. Kupitia ushirikiano huu, tunawatengenezea wateja wetu na wa kampuni za simu fursa kubwa ya kufanya malipo kisasa zaidi," alisisitiza.

Hadi Juni 30, mwaka huu wamiliki wa simu za mkononi nchini walikuwa milioni 53.1 ambao kati yao takriban milioni 33.3 walikuwa wameuganishwa na huduma ya pesa mtandao.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Bidhaa wa Selcom, Gallus Runyeta, mfumo wa msimbo (QR Code) unasaidia sana kurahisisha miamala katika biashara na teknolojia yake imekuwa nyeti kwenye kufanya malipo na kujenga uchumi wa kidijitali.

Alisema QR Code inasaidia sana kuondoa haja ya mtu kutembea na fedha taslimu kwani huduma nyingi muhimu tayari zimeunganishwa na mfumo wake, mathalani maduka makubwa, sheli na hata migahawa.

Aidha, Runyeta alitabainisha kuwa ubia wa Selcom na NMB kwenye hili unasaidia kupanua zaidi mfumo jumuishi wa haraka wa kufanya malipo kidijitali na kuongeza fursa zinazopatikana ndani yake kutokana na wigo mpana wa sehemu na vituo vyao vya malipo.

# Wataka ofisi ya TRA soko la madini

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WAFANYABIASHARA wa madini ya dhahabu katika soko la madini wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameiomba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kufungua ofisi katika soko hilo ili kupata urahisi wa ukaguzi wa nyaraka zao.

Ukaguzi huo ni wa kabla ya usafirishaji wa madini kwenda katika masoko ya kitaifa.

Walidai kuwa, ofisi ya TRA iliyopo ipo katika Mji Mdogo wa Isaka katika Halmashauri ya Msalala, ambapo inachukua umbali wa kilometa 40 kutoka mjini Kahama kufika, kitu ambacho kimekuwa kikisababisha kuachwa na ndege wakati wa usafirishaji wa madini hayo.

Hayo yalibainishwa na Meneja wa Kampuni ya Sub Gold Limited (SGL), Abdulrahim Sangey, wakati akizungumza na vyombo vya habari, na kueleza changamoto ambazo wanakutana nazo wakati wa usafirishaji wa madini kwenda katika masoko ya kimataifa nchi za nje.

Sangey alisema, kutokana na wakaguzi wa mamlaka hiyo kuwa Isaka, wanalazimika kuchelewa usafiri wa ndege zinazokuwa zinatua katika uwanja wa Buzwagi mara mbili kwa wiki, hivyo kusafiri hadi jijini Mwanza kwa njia ya barabara, jambo ambalo ni hatari kupoteza mzigo na linawagharimu fedha nyingi na kuhatarisha usalama wa mali zao.

Naye Emmanuel Sadick, alisema kuna wakati wanasafirisha mzigo nyakati za usiku kwenda jijini Mwanza kwa ajili ya kuwahi ndege zinazokuja kuchukua madini hayo baada ya kuchelewa kupata nyaraka za TRA, jambo ambalo lilikuwa linawezekana kutatuliwa endapo ofisa wa mamlaka hiyo angekuwa ndani ya soko la madini au katika ofisi kuu iliyopo Manispaa ya Kahama.

Meneja wa TRA mkoa wa kikodi wa Kahama, Warioba Kanire, alisema atalifuatia tatizo hilo kwa ukaribu kuangalia namna ya kulitatua ili kuongeza msukumo wa ufanyaji kazi na kuondoa malalamiko ambayo yameanza kuibuka.

Aidha, alisema kwa anavyofahamu, baada ya wafanyabiashara wa madini kumaliza kufunga mali zao kwa ajili ya usafirishaji, maofisa kutoka ofisini kwake wamekuwa wakifika katika soko la madini kukagua nyaraka mbalimbali za usafirishaji wa madini hayo.

Hivi karibuni, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, alifanya ziara katika soko kuu la madini ya dhahabu Manispaa ya Kahama, kwa lengo la kuangalia shughuli ambazo zinaendelea na kuzungumza na wafanyabiashara waliopo na kusikiliza changamoto ambazo zinawakabili.



Mwenyekiti wa kampuni mpya ya bima ya Grand Re Tanzania, Shinganyi Mutasa, akielezea huduma za kampuni hiyo kwa wageni wakati wa hafla ya uzinduzi wake iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijiwe vya NAWEZA vyawawezesha wanaume kuokoa maisha

**Na Mwandishi Wetu**

VIFO vya mama na mtoto kutokana na changamoto za uzazi nchini vitapungua kwa kasi zaidi ikiwa wanaume watatambua nafasi yao katika kuwezesha familia zao kufanya maamuzi sahihi ya kiafya.

Hili limejidhihirisha katika majadiliano na mijadala mbalimbali iliyoibuka jijini Dar es Salaam, kama mwendelezo wa Mkutano wa Mwaka wa Kisayansi wa Huduma za Afya ya Uzazi, Mtoto, Vijana na Lishe, iliyofanyika kuanzia Jumatano hadi Ijumaa.

Caroline Mshanga, kutoka katika mradi wa USAID Tulonge Afya unaoendeshwa na Shirika la Kimataifa la FHI 360 likishirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, aliiambia Nipashe kuwa uhusishwaji mdogo wa wanaume katika kuchochea huduma za afya ya mama na mtoto ikiwamo afya ya uzazi unasababisha kinamama wengi kushindwa kutafuta huduma stahiki.

"Kinamama wanashindwa hata kuhudhuria kliniki wakati wa ujauzito, hawajifungulii katika vituo vya afya, hawatumii njia za kisasa za uzazi wa mpango na wanahofia huduma za msingi sana kama kupima VVU kwa wenzi wote - yote hayo kwa sababu hawapati sapoti ya baba," alisema Mshanga.

Ili kuleta utambuzi na kuchochea ushiriki wa wanaume katika afya ya mama na mtoto, mradi wa USAID Tulonge Afya kupitia Jukwaa la NAWEZA umejipanga kupunguza pengo hili kwa kuwashirikisha wanaume kupitia njia mbalimbali ikiwamo majadiliano ya vikundi pamoja na wenzi wao katika jamii.

Mshanga alisema changamoto iliyojitokeza katika kukutanisha vikundi hivyo ni upatikanaji na ushiriki mdogo wa kinababa, kwani wengi huwa na shughuli nyingi, hali iliyopelekea USAID Tulonge Afya kufanya uamuzi wa kuwatumia wanaume wenyewe kubuni namna mbadala ya kuwakutanisha wajadili changamoto za uzazi na afya na namna ya kushiriki na kuwawezesha wenzi wao kupata huduma.

"Kupitia vyombo vya habari, wanaume wakamenyana katika ubunifu, wazo bora likajitokeza la kuwakutanisha peke yao katika mazingira waliyoyazoea ya Vijiwe vya Kahawa".

Kupitia vijiwe hivi, Mshanga alisema: "Wanaume wanapata nafasi ya kujadiliana na kuelimishana kwa pamoja kuhusu huduma za afya ya uzazi na upatikanaji wake kwa ujumla."

Programu hii ya kuwafikia wanaume vijiweni imeonyesha mafanikio makubwa katika mikoa mitano inayoendesha Vijiwe vya Kahawa vya NAWEZA, ambayo ni Mwanza, Geita, Kigoma, Shinyanga na Tabora.

"Ushiriki wa wanaume katika majadiliano umeongezeka, wanaelimishana na kuhamasishana juu ya huduma hizi za afya ya mama na mtoto na faida zake katika jamii."

"Kupitia vijiwe hivi, takribani wanaume 57,600 wamefikiwa katika kipindi cha miezi sita tu, kuanzia Aprili mpaka Septemba 2021," alisema Mshanga.

USAID Tulonge Afya ni mradi wa miaka mitano unaofadhiliwa na watu wa Marekani kuwezesha mabadiliko ya tabia kwa mtu mmoja mmoja, kaya na jamii kwa ujumla ili Watanzania wengi zaidi watumie huduma mbalimbali za afya na waboreshe ustawi wao binafsi, wa familia zao na wa jamii kwa ujumla.

NAWEZA ni jukwaa wezeshi linalolenga kuhamasisha tabia chanya za kiafya kwa watu wazima wenye umri wa miaka 18 na kuendelea, likitumia mbinu mbalimbali kuifikia jamii na jumbe mahususi za kuhamasisha mambo mbalimbali yakiwamo mahudhurio ya kliniki wakati na baada ya ujauzito.

## PURA yachimba visima 96 vya kutafuta mafuta

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), imesema imefanikiwa kuchimba visima 96 vya kutafuta mafuta, na kwamba kati ya hivyo, 44 vimegundulika kuwa na gesi asilia.

PURA imetoa kauli hiyo katika kuelezea mafanikio mbalimbali iliyoyapata katika kuelekea maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi wa PURA, Charles Sangweni, kati ya visima hiyo 96 vilivyochimbwa, 59 ni vya nchi kavu, 37 baharini huku visima 44 vilivyogundulika kuwa na gesi asilia, nchi kavu viko 16 na baharini viko 28.

Alisema ugunduzi huo umewezesha kuanza kutumika kwa gesi asilia kama chanzo cha nishati hususani kwa kuzalisha umeme viwandani, majumbani na kwenye magari.

"Uzalishaji wa gesi asilia ulianza mwaka 2004 kwa upande wa maeneo ya SongoSongo na mwaka 2006 kwa upande wa Mnazi Bay, hadi sasa kiasi cha gesi kinachozalishwa kinachangia karibu asilimia 60 ya umeme unaozalishwa hapa nchini," alisema Sangweni.

Alisema gesi iliyogunduliwa nchi kavu na ile ya kina kirefu cha bahari ni futi za ujazo trilioni 57.54 ambapo kati ya hizo nchi kavu ni trilioni 10.06 na baharini ni trilioni 47.48.

Sangweni alisema uwapo wa gesi hiyo hususani iliyogunduliwa katika eneo la bahari kuu, kumesababisha serikali kuingia kwenye mazungumzo ya utekelezaji wa mradi wa usindikaji wa gesi hiyo kuwa katika hali ya kimiminika.

Alisema utafutaji huo wa mafuta na gesi unafanyika kupitia mikataba ambayo PURA inaingia na kampuni mbalimbali zinazokuja kuwekeza nchini.

"Hii mikataba huwa tunaingiana kampuni kubwa zinazokuja nchini kuwekeza na wanachokitafuta kikipatikana tunakaa na kukubaliana namna ya kugawana," alisema Sangweni.

"Na kampuni hizi pale zinapokosa kile wanachokitafuta mikataba hiyo imetoa nafasi ya wao kuondoka nchini bila kudai chochote kile na nchi hubaki na taarifa pamoja na takwimu ambazo zinakusanywa wakati wote wa utafutaji.

Sangweni alisema hadi sasa maeneo ambayo tayari wameshayafanyia utafiti ni kilomita za mraba 534,000 ambapo kati ya hizo Km 394,000 zipo nchi kavu na Km 140,000 zipo baharini.

Nipashe
Spotika




10 BORA WALIOFUNGA MABAO MAWILI MCHEZO MMOJA UEFA UK. 12



Harry Kane

# WACHEZAJI WA5 WA KLABU MOJA

**LONDON, England**

SOKA limekuwa tukio kubwa la kibiashara, huku msisitizo mkubwa ukiwekwa kwa nyota wa timu. Uaminifu kwa wachezaji kwa klabu zao ni vigumu kupatikana siku hizi.

Hata hivyo, kuna baadhi ya wachezaji ambao wameweza kubaki kwenye klabu moja licha ya kuwa kwenye wakati mgumu. Wachezaji hawa wamefikia hadhi ya hadithi kwenye klabu zao.

Makala haya tunawaangalia wachezaji watano ambao wamedumu kwenye klabu moja hadi sasa...

**#5. Mark Noble (West Ham United)**

Jina lake la utani ni bwana West Ham, Mark Noble amekuwa mmoja wa wachezaji bora wa klabu hiyo katika nyakati za kisasa.

Noble ni gwiji wa West Ham United. Akiwa ameichezea klabu hiyo kwa mara ya kwanza mwaka 2004, kiungo huyo amecheza mechi 535 katika mashindano yote akiwa na West Ham, akifunga mabao 60 na kutoa pasi za mabao 60. Noble amekuwa na wakati mgumu na mwembamba akiwa na klabu hiyo, baada ya kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa na Ligi Kuu.

Noble anasifika kwa uwezo wake wa kupiga penalti. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 bila shaka alistahili kuichezea England katika nyakati fulani kwenye maisha yake ya soka. Huu ni msimu wa mwisho wa Noble kama mchezaji, kwani alikiri mapema mwaka huu kwamba atatundika daluga mwishoni mwa msimu wa 2021-22.

**#4. Nacho (Real Madrid)**

Ni dhahiri kuwa Nacho hatawahi kuonekana kama beki chaguo la kwanza kwa Real Madrid. Hapo awali ilikuwa Sergio Ramos na Raphael Varane ambao walikuwa mbele yake na sasa ni Eder Militao na David Alaba.

Nacho amekuwa mwaminifu kwa 'Los Blancos' kwa muda sasa. Akiwa zao la akademi ya Real Madrid, aliichezea klabu hiyo kwa mara ya kwanza mwaka 2011. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania amecheza mechi 244 katika mashindano yote akiwa na klabu yake hiyo na amekuwa akitumika katika nafasi mbalimbali za ulinzi.

Akiwa ndiye beki wa kati, Nacho anaweza kucheza katika nafasi zote mbili za nyuma ikihitajika. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, anaonekana kuridhika na maisha yake huko Real Madrid na katika msimu ya hivi karibuni umuhimu wake umeongezeka.

**#3. Harry Kane (Tottenham Hotspur)**

Harry Kane alionekana kuwa tayari kuondoka Tottenham Hotspur msimu wa majira ya joto uliopita pale Manchester City.

Akichukuliwa na wengi kama mshambuliaji bora zaidi duniani, Kane ni fahari ya Tottenham Hotspur. Mchezaji huyo wa kimataifa wa England ni zao la akademi ya klabu hiyo na amecheza mechi 352 katika mashindano yote akiwa na klabu hiyo. Amefunga mabao 228 na kutoa asisti 51 kwa Spurs.

Kane ameshinda Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu England mara tatu na Mchezaji Bora wa Ligi Kuu ya mara moja. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, aliripotiwa kutaka kujiunga na Manchester City msimu wa majira ya joto. Mshambuliaji huyo ameuanza msimu kimya kimya baada ya kukosa kuhama katika ndoto yake.

**#2. Sergio Busquets (Barcelona)**

Bila shaka, kiungo bora zaidi wa ulinzi kuwahi kucheza mchezo huo, Sergio Busquets amepata mafanikio ya ajabu katika kiwango cha juu zaidi.

Busquets ni zao la akademi maarufu ya Barcelona ya La Masia. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania amekuwa na jukumu muhimu kwa Barcelona na nchi yake kwa miaka mingi. Ameshinda mataji manane ya LaLiga, matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Kombe la Dunia na ubingwa wa Ulaya katika maisha yake yote.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, si maarufu kwa uchezaji wake wa kimwili. Busquets ni mwanasoka mwenye akili sana ambaye amejipatia jina kama msomaji bora wa mchezo. Akiwa na kipawa cha kiufundi na kuthaminiwa sana na wachezaji wenzake, Busquets kwa sasa ni nahodha wa Barcelona na timu ya Taifa ya Hispania.

**#1. Thomas Muller (Bayern Munich)**

Thomas Muller ni mwanasoka wa kipekee. Hapendezwi kwa urembo, lakini ni mmoja wa wachezaji bora katika soka la dunia.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, amecheza mechi 599 katika mashindano yote akiwa na Bayern Munich. Amefunga mabao 220 na kutoa asisti 230.

Hajivunii umbo lake, lakini uwezo wa kiufundi wa Muller na kuusoma mchezo umemsaidia kuwa mmoja wa wachezaji bora kabisa wa Bayern Munich.

## ISIKUPITE

MCHEZAJI wa Real Madrid, David Alaba, ndiye beki anayelipwa mshahara mkubwa zaidi duniani kwa sasa akikunja kiasi cha pauni 375,000 kwa wiki, akifuatiwa na Marcelo (Real Madrid) pauni 266,000 na nafasi ya tatu ikishikwa na John Stones wa Manchester City ambaye analipwa pauni 250,000 kwa wiki.



NIPASHE JUMATATU NOVEMBA 22, 2021





# 10 BORA WALIOFUNGA MABAO MAWILI MCHEZO MMOJA UEFA

**ONDON, England**

MICHUANO ya Ligi ya Mabingwa Ulaya imekuwa ikipambwa na wingi wa wachezaji wa kiwango cha kimataifa hasa wafungaji mabao kwa miaka mingi.

Katika miongo mitatu iliyopita ya mashindano hayo, wachezaji wengi wazuri wamefunga mabao mengi, wengine wakifanya hivyo kwa klabu nyingi. Hali hiyo imeendelea katika msimu wa 2021-22.

Katika mechi nne za kwanza za michuano hiyo msimu wa 2021-22, kumekuwa na mabao machache (mchezaji mmoja akifunga mawili kwenye mchezo mmoja). Katika makala haya tunawachambua wachezaji 10 waliofunga mabao mawili kwenye mchezo mmoja.

**#10. Sergio Aguero (Barcelona) - 9**

Sergio Aguero ni mmoja wa wafungaji mahiri zaidi katika mchezo huo kwa sasa na amefunga mabao 41 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Amefunga angalau mara moja katika kila moja ya kampeni zake 12 za awali kwenye kinyang'anyiro hicho, kumi kati ya hizo akiwa na Manchester City.

Sasa akiwa Barcelona, Muargentina huyo alifunga mabao mawili kwa Atletico Madrid katika mechi yake ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya PSV Eindhoven mwaka 2008. Mabao yake mawili ya mwisho alifunga miaka miwili iliyopita, alipofunga kwenye ushindi wa 5-1 wa City dhidi ya Atalanta. .

Hat-trick pekee ya Aguero kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ilikuwa dhidi ya Bayern Munich mwaka 2014.

Msimu uliopita, alicheza fainali yake ya kwanza katika mashindano hayo, lakini aliambulia patupu huku City wakipoteza kwa Chelsea.

**#9. Neymar (PSG) - 9**

Neymar ni mmoja wa wachezaji wenye ustadi zaidi kupamba mchezo huo. Mshindi huyo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2015, aliweka historia kwa kuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao 20 katika mashindano hayo kwa klabu mbili tofauti.

Neymar amefunga angalau mara tatu katika kila kampeni zake nane zilizopita za Ligi ya Mabingwa. Ana idadi kubwa ya mabao 41 na asisti 31 kwenye mashindano hayo.

Baada ya kutofunga bao katika mechi zake tano za kwanza za Ligi ya Mabingwa Ulaya, Neymar alifungua akaunti yake kwa hat-trick dhidi ya Celtic mwaka 2013. Alifunga hat-trick yake ya pili katika mashindano hayo akiwa na PSG miaka mitano baadaye, na kuongeza ya tatu mwaka jana.

**#8. Thierry Henry (Amestaafu) - 10**

Thierry Henry ni mmoja wa wafungaji mahiri zaidi kuwahi kupamba mchezo huo tangu mwanzoni mwa karne hii.

Mfungaji bora wa Arsenal amefunga mara 50 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na klabu tatu tofauti, huku mabao yake mengi akiwa amefunga kwa 'Washikabunduki'. Henry alikuwa sehemu ya Barcelona iliyoshinda taji hilo msimu wa 2008-09, akifunga mara tano msimu huo.

Mfaransa huyo alifunga mabao mawili katika mechi zake nne za kwanza kwenye Ligi ya Mabingwa. Henry kwa mara ya mwisho kufunga mabao mawili kwenye mchezo mmoja wa michuano hiyo ni mwaka 2009.

**#7. Ruud van Nistelrooy (Amestaafu) - 11**

Ruud van Nistelrooy ni mmoja wa wafungaji bora katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ambaye hajawahi kushinda kombe la mashindano hayo.

Raia huyo wa Uholanzi alikuwa mfungaji bora mara tatu wa mashindano hayo wakati akiwa Manchester United, lakini hakuwahi kufika fainali. Katika kipindi chake cha misimu mitano na United, Van Nistelrooy alifunga mabao 35 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kufunga mabao mawili kwa mchezo mmoja kati ya mara 11 ya Van Nistelrooy katika mashindano hayo alifunga akiwa na 'Mashetani Wekundu'. Pia alifunga mabao mawili kwa mchezo mmoja wa michuano hiyo akiwa Real Madrid, ambapo pia alifunga bao lake la 50 kwenye mashindano hayo.

**#6. Filippo Inzaghi (Amestaafu) - 12**

Filippo Inzaghi ni mmoja wa wafungaji mahiri zaidi katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 48 alifunga takriban mabao 50 katika mashindano hayo kwa klabu mbili tofauti, huku mabao mengi akifunga wakati akiwa AC Milan.

Inzaghi alikuwa mchezaji muhimu katika ushindi wa mara mbili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa Milan miaka ya 2000. Yote isipokuwa moja ya mabao yake 12 katika mashindano hayo yalikuja na Rossoneri. Mabao mawili ya Inzaghi katika fainali ya mwaka 2007 dhidi ya Liverpool yaliisaidia Milan kunyakua ushindi wao wa saba.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Italia pia alifunga hat-trick tatu kwenye mashindano hayo, mara moja akiwa na Milan.

**#5. Raul (Amestaafu) - 14**

Raul ni mmoja wa washambuliaji bora katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Gwiji huyo wa Real Madrid alifunga zaidi ya mabao 70 kwenye mashindano hayo, huku mabao yote isipokuwa matano akiifungia 'Los Blancos'.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Hispania ni mmoja wa wachezaji wachanga zaidi kufunga hat-trick ya Ligi ya Mabingwa, baada ya kufanya hivyo mwaka 1995.

Raul alisajili kampeni yake ya mchezaji bora katika mashindano hayo msimu wa 1999-2000, akifunga mara kumi katika kampeni ya ushindi ya Madrid.

**#4. Karim Benzema (Real Madrid) - 17**

Karim Benzema ni mmoja wa wafungaji mahiri zaidi katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mshindi huyo mara nne ni mmoja wa wachezaji wawili pekee waliofunga katika misimu 17 mfululizo ya mashindano hayo. Amefunga angalau mara moja katika kila msimu kwa misimu 12 iliyopita ya Ligi ya Mabingwa.

Amefunga mabao mawili kwa mchezo mara 17 ya Ligi ya Mabingwa isipokuwa mara mbili tu yamepatikana akiwa Real Madrid. Mabao mawili kwa michezo ya hivi karibuni ya Benzema katika mashindano ni wakati Los Blancos wakiishinda Shakhtar Donetsk. Matokeo hayo yalisaidia timu hiyo kwenda kileleni mwa kundi lao.

Benzema pia amefunga hat-trick mbili kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Real Madrid.

**#3. Robert Lewandowski (Bayern Munich) - 20**

Robert Lewandowski ni mmoja wa washambuliaji mahiri waliowahi kupamba Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mshambuliaji huyo wa Bayern Munich alifunga mara 15 katika msimu wa 2019-20 na kushinda taji lake la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Baada ya kufumania nyavu mara tano pekee msimu uliopita, Lewandowski amekuwa wa moto tena msimu huu.

Akiwa na hat-trick yake dhidi ya Benfica, Lewandowski alikuwa mchezaji wa sita kufunga katika mechi yake ya 100 kwenye mashindano hayo. Hiyo ilikuwa hat-trick yake ya nne kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lewandowski ni mchezaji wa sita kufunga katika mechi yake ya 100 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya Thierry Henry, Zlatan Ibrahimovic, Cristiano Ronaldo, Andrea Pirlo na Toni Kroos.

**#2. Lionel Messi (PSG) - 34**

Lionel Messi ni mmoja wa wachezaji bora kuwahi kupamba mchezo huo. Ni mmoja wa wachezaji wawili pekee waliofunga zaidi ya mabao 100 na kufunga hat-trick nane kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Messi ameshinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, amefunga mabao mawili kwenye mchezo mmoja mara 33 akiwa na Barcelona na mara moja akiwa na PSG.

Messi, pamoja na Benzema, ndio wachezaji pekee waliofunga katika misimu 17 mfululizo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#1. Cristiano Ronaldo (Manchester United) - 38**

Cristiano Ronaldo, kama Messi, anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi kucheza mchezo huo.

Akiwa na mabao 139, ndiye mfungaji bora wa muda wote wa mashindano hayo. Mchezaji pekee aliyeshinda mataji matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ronaldo amefunga mabao mengi zaidi kuliko mchezaji yeyote katika historia ya mashindano hayo.

Bao la mwisho la mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, katika Ligi ya Mabingwa Ulaya ilikuwa dhidi ya Atalanta, lilisaidia Manchester United kulazimisha sare.

Kama Messi, Ronaldo pia amefunga hat-trick nane.

Ronaldo amefunga katika mechi zote nne za Ligi ya Mabingwa msimu huu, akifunga mabao matano.




Ronaldo

## Nukuu

"Siku zote huwa nataka kukaa karibu na Lionel Messi, lakini kila ninapopata fursa hiyo, ninaogopa kuzungumza naye na huishia kumwangalia tu, wakati wote [Messi] hutabasamu kwangu," **Ronaldo Jr. (mtoto wa Cristiano Ronaldo).**



"Kwetu ulikuwa mchezo muhimu sana, kabla ya mechi nilizungumza na wachezaji na kuwaambia kwangu huu ulikuwa ni mchezo muhimu zaidi licha ya kwamba siku chache zijazo tutakutana na mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika, tutakutana na Yanga pia, lakini mchezo huu ulikuwa muhimu kwa ajili ya kurudisha hali ya kujiamini kikosini," **Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco baada ya ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Ruvu Shooting**



"Kuna jezi mbili nikivaa najisikia kama shujaa; Jezi ya Brazil na Barcelona. Kwa kuvaa jezi hii, kwa hakika kabisa, najiona mimi ni shujaa na nimekuja hapa kuimarisha klabu," **Dani Alves baada ya kurejea kwa mara nyingine kuitumikia Barcelona**



# LIGI KUU YAREJEA NA REKODI ZA KUMWAGA



Winga machachari wa kulia wa Yanga, Jesus Moloko, akichuana vikali na beki wa kushoto wa Namungo, Edward Charles, kwenye mechi ya raundi ya sita ya Ligi Kuu Tanzania Bara, iliyochezwa Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1.

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya mapumziko ya Kalenda ya FIFA, hatimaye Ligi Kuu Tanzania Bara imerejea tena wiki hii, ikiingia kwenye raundi ya sita.

Mechi zilizochezwa ni Tanzania Prisons iliyokuwa Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga dhidi ya Mbeya Kwanza, Polisi nayo ikiwa nyumbani, Uwanja wa Ushirika, Moshi kuikaribisha Coastal Union, Ruvu Shooting ikaipeleka Simba Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza na Mbeya City ikiialika Mtibwa Sugar, Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Mechi nyingine zilizopigwa ni Kagera Sugar ikiwa Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera ikaikaribisha Geita Gold, Yanga ikawa mgeni wa Namungo, Uwanja wa Ilulu, Lindi, Azam ikajitupa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam kama mgeni wa KMC na Dodoma Jiji ikacheza Uwanja wa Jamhuri Dodoma dhidi ya Biashara United

Ni raundi ambayo imekuwa na matukio mengi ya kushangaza, kufurahisha, kuhuzunisha na kutatanisha, huku rekodi mbalimbali zikiwekwa na kuvunjwa, twende sasa...

**Simba kushinda zaidi ya bao moja**

Kwa mara ya kwanza Simba imeshinda zaidi ya bao moja kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiishindilia Ruvu Shooting mabao 3-1 Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza kwa mabao mawili ya Meddie Kagere na Kibu Denis siku ya Ijumaa.

Kwenye raundi zote tano, Simba ilikuwa ikifunga bao moja moja kwenye michezo mitatu, dhidi ya Dodoma Jiji, Polisi Tanzania na Namungo FC.

Yanga sare ya kwanza Ligi Kuu

Baada ya ushindi wa mechi tano mfululizo, vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakalazimishwa sare ya kwanza kwenye Uwanja wa Ilulu Jumamosi iliyopita.

Ilikuwa ni sare ya bao 1-1, Obrey Chirwa akiifungia Namungo FC na Saido Ntibazonkiza akiifungia Yanga bao la kusawazisha. Yanga ilizifunga Kagera Sugar bao 1-0, Geita Gold 1-0, KMC mabao 2-0, Azam 2-0 na Ruvu Shooting 3-1.

**Rekodi ya Manula yatibuliwa**

Rekodi ya kipa wa Simba, Aishi Manula kutoruhusu mabao kwenye mechi tano, ilivunjika rasmi Jumamosi, baada ya kutunguliwa bao na straika wa zamani wa timu hiyo, Elius Maguri.

Hadi kufikia raundi ya tano, Manula alibaki kuwa ndiye kipa pekee ambaye alikuwa hajaruhusu wavu wake kuguswa. Mechi ya Jumamosi dhidi ya Ruvu Shooting, ndiyo iliyotibua rekodi hiyo licha ya timu yake kupata ushindi wa mabao 3-1.

**Ruvu Shooting 'watoboa tobo'**

Timu ya Ruvu Shooting imejiwekea rekodi ya kuzifunga timu zote mbili kongwe Simba na Yanga mabao ya kwanza.

Novemba 3, mwaka huu, licha ya kufungwa mabao 3-1 dhidi ya Yanga, lakini Shaaban Msala wa Ruvu Shooting alifunga bao lililokuwa la kwanza Yanga kufungwa msimu huu, na kutibua pia rekodi ya kipa raia wa Mali Djigui Diarra ambaye naye wavu wake ulikuwa haujaguswa kwa raundi nne. Ikafanya hivyo kwenye raundi ya tano na kurudia kwa Simba raundi ya sita.

**Kibu Denis afungua akaunti**

Straika wa Simba, Kibu Denis ambaye alicheza kwa dakika zote 90 kwenye mechi ya Jumamosi iliyopita dhidi ya Ruvu Shootinga na kuisaidia kupata ushindi wa mabao 3-1, alifungua akaunti yake ya mabao, akifunga bao lake la kwanza tangu ajiunge na timu hiyo akitokea Mbeya City.

**Coastal, Prisons, Geita zaona mwezi**

TIMU za Coastal Union, Geita Gold na Prisons zimeshinda kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, baada ya raundi tano ngumu za kushindwa kufanya hivyo.

Ikiwa ugenini kwenye Uwanja wa Ushirika Moshi, Coastal Union juzi iliitwanga Polisi Tanzania Bao 1-0, huku Prisons ikiwa nyumbani Uwanja wa Nelson Mandela Sumbawanga, ikiifunga Mbeya Kwanza mabao 2-1. Geita Gold nayo ikiwa ugenini Kaitaba iliiadhiri Kagera Sugar mabao 2-1.

**JE, WAJUA?**



TIMU ya Ruvu Shooting, imekuwa timu ya kwanza msimu huu kuwaokotesha mpira nyavuni makipa wa vigogo vya soka nchini, Simba na Yanga; Aishi Manula na Mali Djigui Diarra licha ya kupoteza kwa mabao 3-1 katika kila mchezo dhidi ya miamba hiyo.








Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, akiwasilisha taarifa ya maendeleo ya wizara hiyo kwa waandishi wa habari jijini Dodoma jana tangu Uhuru wa Tanzania Bara 1961 hiyo ikiwa ni maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru huo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Shirika la Lead latajwa utunzaji mazingira Afrika

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Lead Foundation linalojihusisha na utunzaji wa mazingira mkoani Dodoma, limetangazwa miongoni mwa mashirika 20, yanayoongoza katika miradi ya ustawishaji miti barani Afrika.

Mashirika hayo yalitangazwa rasmi katika mkutano wa mwaka huu wa Umoja wa Mataifa wa mabadiliko ya tabianchi (COP26) uliofanyika hivi karibuni jijini Glasgow, Scotland.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na shirika hilo kwa vyombo vya habari, zaidi ya mashirika 3,200 ya Afrika kutoka katika nchi 31 yalituma maombi kupata fedha kwa ajili ya kuendesha miradi mbalimbali ya kutunza mazingira.

Ambapo katika awamu ya kwanza mashirika 20 ya Afrika yaliyofanya vizuri zaidi katika miradi ya kustawisha miti yamechaguliwa.

Kwa Tanzania shirika pekee lililochaguliwa katika awamu hii ni LEAD Foundation.

"Kuanzia mwaka 2011, LEAD Foundation imefanya kazi kwa karibu na zaidi ya wakulima 120,000 kukomboa ardhi katika maeneo kame ya Tanzania," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Ilisema kwa pamoja wameweza kustawisha zaidi ya miti milioni tisa ya asili na kukomboa zaidi ya hekta 124,000 za ardhi kwa kutumia njia mbalimbali ikiwamo njia ya Kilimo Msitu ya Kisiki Hai (Farmer Managed Natural Regeneration - FMNR) pamoja na njia ya Uvunaji wa Maji ya Mvua (Rainwater Harvesting - RWH).

Kwa msaada wa fedha, LEAD Foundation inategemea kuendeleza jitihada zake za kukomboa mazingira katika maeneo kame ambayo yalikuwa bado hayajafikiwa katika mkoa wa Dodoma.

Aidha, shirika hilo litawasaidia wakulima na wafugaji kustawisha miti ili kuondokana na athari za ukame, mmomonyoko wa udongo pamoja na kurutubisha ardhi ya mashamba na malisho ya mifugo.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa miaka sita iliyopita, viongozi wa Afrika walitambua kuwa uharibifu mkubwa wa takriban asilimia 65 ya ardhi ya kilimo katika bara hilo ni tishio kwa uchumi na maisha ya mamilioni ya wakulima.

Ilisema kuwa waligundua hivyo kutokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi yanayosababisha uzalishaji mdogo wa mazao, mvua zisizo tabirika na vipindi virefu vya ukame vinavyofanya maisha ya mamilioni ya wakulima kuwa magumu na hivyo kusababisha ongezeko kubwa la watu wanaoacha shughuli za kilimo na kukimbilia mijini kutafuta riziki.

"Hii ndio sababu mwaka 2015 nchi za Afrika ziliahidi kukomboa hekta milioni 100 za mazingira na ardhi iliyochakaa kufikia mwaka 2030 kupitia Mpango wa AFR100," ilibainisha taarifa hiyo

Kutokana na hali hiyo, maelfu ya mashirika madogo ya kiafrika yameibua miradi na njia mbalimbali za kibunifu za kukomboa mazingira ili kuleta matokeo chanya kwa faida ya Afrika ya kesho.

"Inakadiriwa kuwa wakulima barani Afrika wanamiliki karibu asilimia 70 ya ardhi yote ya Afrika," ilieleza.

Kadhalika, ilisema kuwa hatuwezi kufanikiwa kufikia malengo ya kuachana na uchafuzi wa hewa ukaa kufikia mwaka 2050 kama tutapuuzia jitihada za mashirika madogo yanayofanya miradi ya kukomboa mazingira kwa kushirikiana kwa karibu na wakulima.

"Hii ndio sababu kampuni mbalimbali kubwa duniani zimeiwezesha TerraFund kwa ajili ya Mpango wa AFR100 kuyasaidia mashirika ya Afrika na yanayoongozwa na Waafrika wenyewe yaliyoibuka kidedea katika kustawisha miti barani Afrika."

Aidha, katika awamu ya kwanza kampuni mbalimbali zimeahidi kutoa zaidi ya Dola za kimarekani milioni 135, zitakazowezesha kukomboa hekta milioni 20 kabla ya mwaka 2026.

Vilevile, mpango wa AFR100 umeyataka mataifa yaliyoendelea kuhakikisha yanaipatia Afrika angalau Dola za kimarekani bilioni mbili kabla ya mkutano ujao wa COP27 mwakani.

# Maofisa ugani watakiwa kutoa taarifa sahihi za hali ya hewa

**Na Peter Mkwavila,** KONGWA

MAOFISA ugani wameshauriwa kutoa taarifa sahihi za hali ya hewa kwa wakulima ili waweze kulima kilimo chenye tija na endelevu badala ya kile cha mazoea.

Ushauri huo ulitolewa na mtaalamu wa hali ya hewa kutoka Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Mponda Malozo.

Malozo alisema hayo alipokuwa akitoa mafunzo kwa maofisa ugani na wakulima kuhusu utabiri wa hali ya hewa na ushauri wa ngazi ya wilaya kwa msimu wa kilimo 2021/2022 yaliyofanyika Wilaya ya Kongwa.

Mafunzo hayo ambayo yamedhaminiwa na Shirika na Msaada wa Watu wa Marekali (USAID) pamoja na USDA kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo.

Aidha, maofisa hao wametakiwa kupeleka taarifa zilizo sahihi kwa wakulima vijijini ili walime kilimo chenye tija na endelevu kwa wakati. "Tusichukulie utendaji wetu wa kazi kwa mazoea katika kutoa taarifa za hali ya hewa kwa wakulima, tumieni mbinu mbalimbali mlizojifunza ili wakulima hao waweze kufikia kuwaamini na wao waweze kufikia malengo,"alisema.

Malozo alisema kuwa bado kuna changamoto kwa wakulima katika kupata taarifa sahihi za hali ya hewa kwa wakati kutokana na walio wengi kutokuwa na mawasiliano kama vile simu za viganjani, radio, luninga na mitandao ya kijamii hali ambayo imekuwa ikisababisha kuchelewa kuwafikia taarifa za utabiri wa hali ya hewa.

Naye Ramadhani Omary kutoka makao makuu ya Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), aliwataka wakulima na wafugaji kupata ushauri zaidi kutoka kwa maofisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa kwa saa 24 siku 10 hadi mwezi.

Aidha, aliwashauri wakulima kuhakikisha wanapanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu, huku pia wakitakiwa kutumia teknolojia ya uvunaji maji ya mvua na wafugaji wafuate njia bora za ufugaji ikiwamo kupanda malisho na uhifadhi.

# Wahitimu CBE wajengewa uwezo kujiajiri

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE) kimezindua kanuni atamizi za biashara za ufundishaji uwanagenzi ikiwa ni njia ya kuwajenga wahitimu wa chuo hicho uwezo wa kujiajiri.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax, akizungumza juzi baada ya uzinduzi huo uliofanyika katika kongamano la wanataaluma alisema hatua hiyo ni muhimu kwani ni nyenzo ya kutoa elimu kwa vitendo jambo ambalo litawafanya wahitimu kuwa tayari kujiajiri.

"Tunapopata fursa za masomo mawazo ya wanafunzi ni kuwa nikimaliza hapa nikapate ajira, lakini kwa kuanza kufundisha kwa vitendo kutasiadia kuwaandaa wahitimu wetu hata kama hajamaliza masomo tayari anakuwa ameandaliwa kujiajiri au akihitimu na huu ni mfano wa kuigwa na vyuo vingine," alisema.

Aidha, Dk. Tax aliutaka uongozi wa CBE kuzitumia vizuri kanuni hizo na kuzifanya kipaumbele cha chuo kwa sababu zinakwenda kutatua changamoto ya ajira ambayo bado ni kero nchini.

"Kwa sasa kuna matatizo mengi, kama serikali tunajaribu kupambana na umaskini na ukosefu wa ajira, hivyo hii itakuwa na mchango mkubwa sana katika kupambana na tatizo la ajira na vijana wanaweza kujiajiri," alisisitiza.

Alisema takwimu alizonazo zinaonyesha asilimia 60 ya wahitimu wa Chuo cha CBE wamejiajiri.

Aidha, Dk. Tax alisema serikali inathamini umuhimu wa elimu katika ngazi zote kama inavyoonekana katika sera, mikakati na programu za serikali na kusisitiza Watanzania kuiunga mkono serikali ambayo inadhamira ya kuwaletea maendeleo.

Mwenyekiti wa Bodi ya CBE, Prof. Wineaster Anderson, aliwataka wafanyakazi wa CBE, kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma na kuepuka vitendo vinavyoleta majaribu.

Mkuu wa Chuo cha CBE, Prof. Emanuel Mjema, alisema hatua ya kuandaa kanuni ni kuhakikisha wanaongeza ufundishaji kwa kuondokana na ufundishaji wa nadharia pekee na kufundisha kwa vitendo.

Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Tandi Lwago, alisema kongamano la wanataaluma limetanguliwa na kongamano la kitaaluma ambalo lilihudhuliwa na watafiti kutoka ndani na nje ya nchi, wafanyabiashara na wanazuoni zaidi ya 300.



# Polisi: Salimisheni silaha zisizosajiliwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limewataka wananchi wote wanaomiliki silaha za moto kinyume cha sheria kuzisalimisha katika ofisi za serikali kabla ya Novemba 30, mwaka huu.

Jeshi hilo limesema kwamba limetoa muda huo ili kuepuka wahusika kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, aliyasema hayo juzi alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari, ambapo alisema zoezi hilo lilianza Novemba mosi mwaka huu.

Alisema zoezi hilo ni utekelezaji wa agizo la Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alilolitoa Oktoba 29 mwaka huu, kwa lengo la kudhibiti matukio ya uhalifu hasa matumizi mabaya ya silaha hizo.

Alisema silaha hizo zinatakiwa kuwasilisha kwenye ofisi za Serikali za Mitaa na Ofisi za Watendaji wa Kata kila siku za kazi kuanzia saa 02:00 asubuhi mpaka saa 10:00 jioni.

Alisema mtu yeyote ambaye atasalimisha silaha hizo kwa hiyari, hatachukuliwa hatua yoyote isipokuwa wale watakaokutwa nazo wakati wa msako utakaofanyika baada ya Novemba 30.

"Kwa zile silaha ambazo wamiliki wake wamefariki ama wamepoteza sifa za kumilikishwa silaha, wanatakiwa kufika Kituo cha Polisi ili amilikishwe kihalali silaha hiyo ama taratibu zingine zinazotakiwa kwa mujibu wa sheria," alisema Kamanda Matei.

Kamanda Matei aliwataka viongozi wote wa serikali, dini pamoja na viongozi wa mila kushiriki katika zoezi hilo kwa kuwahamasisha wananchi wanaomiliki silaha hizo ikiwa ni pamoja na wao wenyewe kuanza kuziwasilisha.

Katika hatua nyingine Kamanda Matei aliwataka wananchi wa mkoa huo kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi kudhibiti matukio ya uhalifu katika kipindi hiki cha kuelekea mwisho wa mwaka kwa madai kuwa matukio hayo huwa yanaongezeka.

Vilevile, alisema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa usalama barabarani wataendelea kudhibiti matukio ya ajali za barabarani kwa kuhakikisha madereva wanafuata sheria.



Mratibu wa Utafiti na Ubunifu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole, jijini Mbeya, Dk. Emmanuel Chilagane, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mipango ya utafiti wa taasisi hiyo uliofanyika mwaka 2020 wakati wa mkutano wa watafiti na wadau wa utafiti uliofanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA:NEBART MSOKWA**

# TARI yajitosa kukabili mabadiliko ya tabianchi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, imejitosa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, kwa kuzalisha mbegu na teknolojia za kisasa zitakazowasaidia wakulima kuepuka athari mabadiliko hayo.

Hivi karibuni, Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) ilitangaza kuwa mwaka huu kutakuwa na uhaba wa mvua katika baadhi ya maeneo, hivyo ikawataka wananchi hasa wakulima kuanza kuchukua tahadhari za kuepuka athari za hali hiyo.

Akizungumza wakati wa mkutano wa watafiti na wadau wa utafiti wa kilimo uliofanyika jijini Mbeya, Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema taasisi hiyo imezalisha mbegu za mazao mbalimbali ambazo zinahimili ukame na zinazokomaa kwa muda mfupi.

Alisema mbegu hizo pamoja na teknolojia za uzalishaji zilishaandaliwa kwa ajili ya kujihami na matukio ya uhaba wa mvua endapo yatatokea na kwamba kwa sasa wameamua kuanza kuzitumia baada ya TMA kutangaza uwepo wa uhaba wa mvua.

"Huwezi kuanza kutafuta silaha wakati tayari adui yuko ndani bali unaziandaa kwa ajili ya tahadhari, kwa hiyo hata sisi tulishaandaa teknolojia za kujihami, tuna mbegu za mahindi, maharage, ngano na mazao mengine ambayo yanahimili mvua chache hivyo tunawashauri wakulima wazitumie kwa mwaka huu," alisema Dk. Bucheyeki.

Aliwataka wakulima kwenda katika taasisi hiyo kwa ajili ya kujifunza teknolojia hiyo kabla mvua haijaanza kunyesha na kwamba kwa walio mbali na taasisi hiyo wanatakiwa waende katika idara za kilimo za halmashauri zao ambazo alisema wanashirikiana nazo.

Meneja wa TARI Kituo cha Kifyulilo kilichoko mkoani Iringa, Dk. Ndabhemeye Mlengela, alisema serikali imewekeza fedha nyingi kwa ajili ya utafiti wa mbegu na teknolojia za kilimo ili kuwasaidia wakulima kuongeza tija.

Alisema kwa sasa wakulima wanatakiwa wahakikishe wanazitumia teknolojia hizo pamoja na mbegu zinazozalishwa ili wazalishe kwa tija mazao kwa ajili ya kujitosheleza kwa chakula pamoja na kuuza ziada na kujiongezea kipato.

Alisema kuwa teknolojia zilizozalishwa na taasisi hiyo zitawasaidia wakulima kupata tija pamoja na uwepo wa tatizo la uhaba wa mvua unaotarajiwa kutokea mwaka huu.

"Endapo wakulima hawatatumia mbegu na teknolojia za kisasa kuna hatari ya kupata tija ndogo sana kwenye kilimo, sisi tumefanya kazi ya utafiti na imebaki kwa wakulima kuzitumia," alisema Dk. Mlengela.

Mratibu wa Utafiti na Ubunifu wa TARI Uyole, Dk. Emmanuel Chilagane, alisema katika mkutano huo watafiti waliwasilisha maandiko 19 ya utafiti yenye lengo la kuboresha kilimo nchini yakiwamo yanayoangazia mabadiliko ya tabianchi.

Vilevile, alisema watafiti waliwasilisha taarifa za miradi 23 ya utafiti ambayo ilifanyika katika msimu wa kilimo uliopita na kwamba watafiti walitakiwa kujadiliana taarifa hizo ili kuziboresha kwa ajili ya utekelezaji.

Mratibu wa Uzalishaji na Biashara kutoka TARI Makao Makuu, Kissa Mwaisoba, aliwataka watafiti kuendelea kufanya tafiti mbalimbali za kilimo ili kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao.

Alisema kilimo ni sekta muhimu kutokana na kuwa chanzo kikuu cha chakula kwa binadamu pamoja na malighafi kwa ajili ya viwanda na kwamba sekta hiyo ni miongoni mwa vyanzo vya mapato ya nchi.

Watafiti waliohudhuria mkutano huo walikuwa ni wa kutoka katika vituo vya TARI vya mikoa ya Mbeya, Iringa, Dodoma na Dar es Salaam.

# Wakulima wadanganyifu tumbaku wamkera RC

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amekerwa na tabia ya baadhi ya wakulima wa tumbaku wilayani Chunya kuchanganya madaraja ya tumbaku wakati wa kufunga na kuuza.

Homera amesema kwamba kitendo hicho kinasababisha kuharibika kwa soko la zao hilo.

Homera alionyesha kukerwa na tabia hiyo alipokuwa anazungumza na wakulima wa tumbaku kutoka katika vyama vya msingi 18 kwenye mkutano uliofanyika katika Kata ya Lupatingatinga ambapo aliwataka wakulima hao kuacha tabia hiyo.

Alisema baadhi ya wakulima hao huwa wanaweka mawe katikati ya mitumba ya tumbaku ili kuongeza uzito jambo ambalo alisema ni udanganyifu unaoharibu soko la tumbaku kwa madai kuwa wanunuzi ni lazima wakaguwe.

"Tumbaku inayolimwa Chunya ni nzuri kuliko inayolimwa kwenye maeneo mengine lakini tatizo lililopo ni wakulima kuchanganya madaraja jambo ambalo linashusha ubora na hivyo soko kuwa chini," alisema Homera.

Katika hatua nyingine, Homera aliwatahadharisha wakulima kuacha tabia ya kutorosha tumbaku na kwenda kuuza kwenye mikoa mingine akidai kuwa kitendo hicho ni kinyume na utaratibu wa uuzaji wa zao hilo.

Alisema kwa yeyote ambaye atakamatwa akifanya biashara hiyo atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kupelekwa mahakamani na tumbaku yake kutaifishwa ili iwe fundisho kwa wakulima wengine wenye tabia kama hiyo.

Alisema tumbaku yote inatakiwa kuuzwa kwa njia ya ushirika ndani ya wilaya husika kwa madai kuwa kila mkulima anatakiwa awe mwanachama wa chama cha msingi cha wakulima wa zao hilo.

Awali akitoa taarifa ya kilimo cha Tumbaku wilayani humo, Ofisa Ushirika kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Mkoa wa Mbeya, Bielery Malila, alisema tatizo la wakulima kuchanganya madaraja limekuwa kubwa ndani ya wilaya hiyo.

Alisema kutokana na tatizo hilo msimu wa kilimo uliopita, baadhi ya wanunuzi waliokuwa wamenunua tumbaku hiyo waliirejesha kwenye vyama vya msingi na kusababisha hasara kwa wakulima hali ambayo ilizaa tatizo lingine la wakulima kushindwa kurejesha mikopo.

Alisema tatizo hilo pia liliviongezea vyama vya msingi gharama za kuandaa upya masoko ya wakulima waliorejeshewa tumbaku jambo ambalo alidai limekuwa likirudisha nyuma wakulima.

"Kutokana na tatizo hili, Bodi ya Tumbaku na Chama cha Kikuu cha Wakulima wa Tumbaku Wilaya ya Chunya (CHUTCU) kuendelea kutoa elimu ya uchambuaji na ufungaji wa tumbaku na tunawataka wakulima wawe tayari kupokea elimu hii," alisema Malila.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, alisema msimu uliopita waliwakamata baadhi ya wakulima wakitorosha tumbaku na tumbaku hiyo ikataifishwa.

Alisema endapo mkulima yeyote atakamatwa tena akifanya uhuni huo, ni lazima hatua za kisheria zitaendelea kuchukuliwa kwa madai kuwa baadhi yao wanakopeshwa pembejeo na vyama vyao lakini wanatorosha tumbaku ili kuepuka kulipa madeni hayo.



# Mapenzi ya jinsia moja, ukahaba tishio Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UNGUJA imetejwa kuwa inaongoza kuwa na idadi kubwa ya wanawake wanaofanya biashara ya kuuza miili yao pamoja na wanaume wanaofanya mapenzi ya jinsia moja ikilinganishwa na Pemba.

Akizungumza na waandishi wa habari Mjini Zanzibar, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Salum Mkuya, alisema jumla ya wanawake 5,554 wanauza miili yao Zanzibar ambapo Unguja ni 4,854 na Pemba ni 700.

Alisema idadi ya wanaume wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja Zanzibar ni 3,300 ambapo Unguja ni 3,300 wakati Pemba ni 300.

Alisema asilimia kubwa ya maambukizo ya Virusi vya Ukimwi yapo kwa makundi maalum yakiwamo wanawake wanaofanya biashara ya miili yao ambayo ni asilimia 12, wanaume wanaofanya mapenzi ya jinsia moja asilimia 5 na wanaotumia dawa za kulevya kwa kujidunga sindano asilimia 5.1.

Alieleza takwimu hizo ni kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Wizara ya Afya Zanzibar mwaka 2018 ambapo watu 2,600 Zanzibar wanatumia dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga sindano Unguja ni 2,200 na Pemba ni 400.

Alisema wizara yake imeendelea na jitihada za kuyafikia makundi hayo maalum kwa lengo la kuyapa elimu na kupima maambukizio ya VVU na hadi kufikia Septemba mwaka huu, jumla ya watu 10,378 wa makundi maalum wamefikiwa na 6,424 walikubali kupima VVU ambapo 69 waligundulika na maambukizi ya VVU.

Waziri huyo alieleza kuwa kutoka Julai mwaka jana hadi Juni mwaka huu, jumla ya wajawazito 56,165 wamefanyiwa uchunguzi wa VVU ambapo kati yao 104 waligundulika na VVU, watoto 381 waliozaliwa walichunguzwa afya zao na watano waligundulika na maambukizi ya virusi hivyo.

"Katika kudhibiti maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto kiwango cha maambukizi chini ya asilimia tano kinachukuliwa kama ni ishara ya ufanisi katika kuwalinda watoto dhidi ya maambukizi kutoka kwa mama zao," alisema Dk. Saada.

Alieleza katika kuibua mbinu za kudhibiti mazingira hatarishi yanayoweza kuchangia kuongezeka kwa maambukizi ya VVU, wizara yake kwa kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, imeweka utaratibu kudhibiti upigaji wa ngoma na muziki katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba kwa kuzuia vibali.

Alisema pia wamefungia baa na nyumba za kulala wageni na hoteli zinazoendeshwa kinyume cha utaratibu au zinazochochea tabia hatarishi pamoja na kudhibiti bandari zisizorasmi kwa kusimamia uingiaji wa wageni wasiokuwa na shughuli zinazoeleweka.

Aidha, alisema Zanzibar bado inakabiliwa na tatizo la unyanyapaa kwa wanaoishi na VVU, licha ya elimu inayotolewa kwa jamii, hivyo aliwasisitiza wananchi kuacha unyanyapaa.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya, akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Migombani Mjini Zanzibar, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya wizara hiyo kwa muda wa mwaka mmoja.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Masheha wapewa jukumu udhibiti uchimbaji mchanga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kaskazini' B' Unguja, Hamid Seif Said, amewataka masheha kufanya doria za mara kwa mara katika maeneo yanayochimbwa mchanga kinyume cha utaratibu ili kuzuia uharibifu wa mazingira.

Aliyasema hayo huko Kisongoni wilayani humo alipotembelea bwawa la maji ya kumwagilia mpunga katika Bonde la Kibokwa.

Alisema doria za mara kwa mara za masheha na kamati zao zitasaidia kupunguza uchimbaji wa mchanga kiholela na kuwataka masheha hao watakapomwona mtu anayechimba mchanga kinyume cha sheria wafikishe taarifa katika vyombo husika ili kuchukuliwa hatua.

Aidha, aliwataka masheha hao kuunda kamati za ulinzi katika shehia zao ili kuwasaidia katika kufanya doria hizo.

Aliwataka wananchi waache kuwaficha wahalifu wa uharibifu wa mazingira badala yake kuwaripoti katika vyombo vya sheria.

Aliyasema hayo baada ya kupata malalamiko kwa baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Kisongoni kuwa sehemu lililojengwa bwawa hilo linachimbwa mchanga na baadhi yao wakidai kuwa bado hawajalipwa fidia ya miti yao iliyokatwa kwa ajili ya bwawa hilo.

Akitoa malalamiko ya wananchi mbele ya Mkuu wa Wilaya huyo, Vuai Muhidini Mzee, alisema pamoja na kujengewa bwawa la Kisongoni katika shehia za Kinyasini, Mgambo na Kisongoni, lakini wanashindwa kufika katika mashamba yao kutokana na kukosekana daraja la kuziunganisha shehia hizo.

Alieleza kwa kutegemea kilimo katika kuendesha maisha yao, lakini kwa sasa hali imekuwa ngumu na hawezi kufika sehemu husika kwa ajili ya kuendeleza kilimo.

Bwawa la Kisongoni lililojengwa kwa ajili ya kumwagilia mpunga, bado linakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo kukosekana kwa walinzi, uzio na madaraja ya kuunganisha shehia za Kinyasini, Kisongoni na Mgambo.

# Mahakama ya udhalilishaji yaleta unafuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUANZISHWA mahakama maalum ya kushughulikia kesi za udhalilishaji Zanzibar, kumewahamasisha watu wengi kuongeza juhudi za kupambana na udhalilishaji hasa wa watoto.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wanaharakati wa kutetea haki za wanawake na watoto walisema mwamko huo unaonekana kutoa matumaini ya kusaidia kupunguza au kutokomeza vitendo hivyo ambavyo kasi yake ilikuwa kubwa sehemu mbalimbali za Unguja na Pemba.

Mahakama hiyo iliyoanzishwa, ilianza kufanyakazi rasmi mwanzoni mwa Julai mwaka huu, baada ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuagiza kufuatia kushamiri vitendo hivyo.

Fatma Juma, alisema kufanyike marekebisho ya sheria ya mtoto ili umri wa mtoto uwe na kikomo miaka 14 badala ya 18 kutokana na kuonekana kesi nyingi zinazoripotiwa mahakamani huanzia na watoto wa miaka 15 ambao tayari wanajitambua.

"Jamii ielimishwe umuhimu wa kuendelea na kesi bila ya kukatisha njiani na familia ziache kutafuta suluhu nje ya mahakama," alisema.

Katika ufuatiliaji wa kutathmini kesi hizo za udhalilishaji mahakamani kwa Julai hadi Septemba mwaka huu, imebainika kuwa kuna kesi 22 kwa Mahakama ya Mkoa wa Kusini iliyopo Mwera na kesi 14 kwa Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja iliyopo Mahonda na kesi 77 Mahakama ya Mkoa wa Mjini Unguja iliyopo Vuga.

Hakimu wa Mahakama Mkoa Mwera, Khamis Ali Silima, aliiambia Nipashe kwamba jumla ya kesi 16 kwa Mahakama hiyo Mwera Unguja zimeshapatiwa hukumu katika kipindi cha Julai hadi Septemba mwaka huu.

Aidha, jumla ya kesi tano katika Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja Mahonda nazo zimetolewa hukumu, kwa mujibu wa Hakimu wa Mahakama hiyo, Mohammed Subeit na kesi saba zimetolewa hukumu kwa Mahakama ya Mkoa Vuga kwa mujibu wa Hakimu wa Mahakama hiyo, Yesaya Kayange.

Mahakimu hao walisema miongoni mwa kesi hizo zipo zilizotolewa hukumu kwa muda mrefu zaidi ya mwaka mmoja na zipo zilizotolewa hukumu kwa muda mfupi ambapo tokea kuanzishwa kwa Mahakama Maalumu ya udhalilishaji.

Alisema moja ya sababu ambayo inasababisha kesi kusikilizwa kwa haraka ni jinsi mashahidi wanavyopatikana kwa wingi kwenda kutoa ushahidi mahakamani na sababu nyingine ni kesi zinapofanyiwa uchunguzi haraka polisi huwa hazichukui muda mrefu kukamilishwa na kutolewa hukumu Mahakamani.

Dk. Mzuri Issa, Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania TAMWA ofisi ya Zanzibar, alisema elimu iendelee kutolewa kwa umma kuacha kutoa talaka ovyo na tatizo kubwa limeonekana wazazi wanapoachana watoto hukosa matunzo, hivyo kushawishika na kufanyiwa udhalilishaji.

Aidha, alisema familia zichukue wajibu wake wa kuwalea na kuwatunza watoto ili kuepukana na udhalilishaji ikiwamo ubakaji, ulawiti na kutoroshwa.

# Ofisi za ardhi mikoa zaongeza bajeti kwa 44%

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

TANGU kuanzishwa kwa ofisi za ardhi za mikoa, bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeongezeka kutoka shilingi bilioni 67 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 mpaka kufikia shilingi bilioni 97 mwaka 2021/2022.

Hilo ni ongezeko la asilimia 44 na kuyafanya majukumu ya wahasibu kuongezeka maradufu katika kutekeleza kazi za wizara kwenye ofisi za mikoa na halmashauri zake.

Hayo yamebainishwa juzi jijini Dodoma na Mhasibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Walter Lungu, wakati akifungua kikao kazi cha kujadili changamoto na namna ya kuongeza ufanisi katika utendaji kazi kwa wahasibu ili wawe sehemu ya kuchangia kufanikisha lengo la mapato ambapo Wizara ya Ardhi imepangiwa kukusanya shilingi bilioni 221 kutoka Sh. bilioni 180 za mwaka wa fedha uliopita 2021/2021.

Pamoja na masuala mengine ya kiutendaji, Lungu alizungumzia suala la wahasibu kujiendeleza kwa lengo la kuhakikisha huduma katika sekta ya ardhi inatolewa kwa wepesi, haraka na kwa ufanisi wa hali ya juu.

"Kutokana na maendeleo kwenye teknolojia kuathiri kada mbalimbali katika utumishi wa umma ikiwamo kada ya wahasibu mnatakiwa kujiendeleza ili kuhakikisha huduma inatolewa kwa wepesi, haraka na kwa ufanisi wa hali ya juu," alisema Lungu.

Akimwakilisha Kamishna wa Ardhi nchini katika kikao hicho, Kamishna wa Ardhi Msaidizi Usimamizi na Uratibu, Wilson Luge, aliwataka wahasibu kuhakikisha wanafanya kazi kwa weledi bila ya kuhofia cheo au nani alitoa maelekezo kwani hoja ya uhasibu itakapokuja kuhusu matumizi yasiyo rasmi ya fedha haitaangalia nani alitoa maelekezo bali ni utaratibu gani ulitumika katika kutekeleza majukumu na kama sheria na taratibu zilifuatwa kwenye taaluma ya uhasibu.

Pia Luge aliwaomba wahasibu washirikiane na makamishna wa mikoa wakati wa kuandaa bajeti ili kuepuka makosa yanayojitokeza mara kwa mara aliyoyaeleza kuwa, wakati mwingine yanakwamisha utengaji fedha kwa majukumu yaliyokusudiwa.

Akitoa salamu kwa niaba ya Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Ardhi, Antony Mgeni ambaye ni Ofisa Rasilimali Watu Mwandamizi, alisisitiza umuhimu wa wahasibu kuheshimu misingi ya taaluma sambamba na kujikita katika maadili kwa lengo la kuepusha makosa ya kitaaluma yanayoweza kujitokeza.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbalo (kushoto), akitalii Hifadhi ya Taifa ya Tarangire kwenye kumbukizi ya miaka mitatu ya jeshi usu la uhifadhi, wanyamapori na misitu, kulia ni Meneja wa Kuro Tree Tops Lodge, Julius Kariuki, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Kampuni mpya bima kutoa huduma nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya bima ya Grand Re ya barani Afrika, imezindua huduma zake nchini.

Akizungumza kwenye hafla ya uzinduzi huo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti wa kampuni hiyo, Shingayi Mutasa, alisema inatoa huduma za bima ya uhakika na za kifedha hususani katika nchi zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara kupitia kufanya kazi pamoja kwa ubunifu, uadilifu, kuaminika na shauku ya kutoa huduma bora kwa wateja.

Alisema Grand Re Tanzania, iliyoanza kutoa huduma nchini katika siku za karibuni ikilenga soko la nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, itatoa huduma mbalimbali za bima zikiwamo bima za muda mfupi za kukabiliana na majanga ya usafiri wa anga, moto, magari na nyinginezo.

Kwa mujibu wa Mutasa, Grand Re Tanzania inajihusisha na ushauri wa kitaalamu wa kukabiliana na majanga mbalimbali, usalama wa kifedha lengo likiwa ni kuwawezesha wateja wake kufanya biashara zao kwa kujiamini zaidi na kupata mafanikio katika biashara zao.

Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Mussa Juma, ambaye alikuwa mgeni rasmi, aliipongeza kampuni ya Grand Re, kwa kufungua tawi Tanzania na kuongeza kuwa anaamini kuwa itatumia uzoefu wake mkubwa na utaalamu kuzidi kuboresha huduma katika sekta ya bima nchini.

Grand Re, ilianzishwa rasmi mwaka wa 2005, ikiwa na lengo la kutoa huduma bora za bima za aina mbalimbali katika soko la Afrika hususani katika nchi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara.

# Halmashauri zatenga fedha kwa uhifadhi misitu vijijini

**Na Christina Haule, LINDI**

HALMASHAURI za wilaya nchini zimeanza kutenga fedha kusaidia vijiji kuhifadhi misitu iliyopo na kuacha kujihusisha na kilimo, mifugo bila kufuata taratibu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Tina Sekambo, alisema jana kuwa halmashauri hiyo imetenga shilingi milioni 30 katika bajeti yake ya mwaka wa fedha 2021/22, ili kusaidia vijiji kuelimika na kuona umuhimu wa misitu katika mpango wa usimamizi shirikishi wa misitu kwa jamii (USMJ) fedha ambazo tayari zimeshaanza kutumika.

Sekambo alisema wanaendelea kuelimisha wananchi na kuwataka kutambua kuwa wakati wote wanapaswa kuwa wasimamizi wazuri wa misitu kwa kufuata kanuni zilizowekwa.

Alisema halmashauri hiyo ina jumla ya vijiji 76 ambavyo vimeshaingizwa katika mpango wa matumizi bora ya ardhi, ambapo vinapaswa kusimamia sheria zilizopo za usimamizi shirikishi wa misitu huku zingine zikiwa tayari zimeshaomba kuanzisha usimamizi shirikishi wa misitu (USM).

Naye Mkuu wa Wilaya ya Liwale, Judith Nguli, aliwaomba wataalamu wa masuala ya uhifadhi na usimamizi wa misitu kufika wilayani humo kutoa elimu ya uhifadhi wa misitu ili kuleta faida kufuatia robo tatu ya wilaya hiyo kubebwa na misitu ya asili.

Alisema misitu huleta faida kubwa kwa jamii hasa pale inapotunzwa kwa manufaa ya wanavijiji na kwamba suala la ukataji miti wilayani humo linatokana na uasili uliopo kwa wakazi wa hapo unaotokana na kilimo cha kuhamahama sambamba na wananchi kuona eneo la matumizi bado ni kubwa kwao.

Aidha, Nguli alifafanua kuwa ikiwa wadau wa misitu wataongeza nguvu kutoa elimu wilayani humo anaimani suala la uhifadhi wa misitu litaweza kusimamiwa vyema na jamii yenyewe.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro, Hasani Njama, alisema halmashauri hiyo imetenga shilingi milioni 5 katika bajeti yake ya mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya kuboresha elimu kwa jamii juu ya masuala ya USMJ.

Alisema fedha hizo zitatumika katika kutoa elimu ya utunzaji na kupanga maeneo ya misitu kwa kuhakikisha jamii inatekeleza sheria ndogo za usimamizi wa misitu zilizopo.

Mtendaji wa Kata ya Kinda wilayani Mvomero, Fortunata George, alisema wananchi wanapaswa kupata uelewa zaidi juu ya ushirikishwaji wa misitu ambapo kwa kushirikiana na viongozi wa kamati za misitu wameahidi kutumia miaka 2-3 kuwakatia bima ya afya CHF wakazi wote wa kata hiyo fedha ambazo zitatokana na manufaa ya mradi huo.

Mradi wa CoForEST unaotarajiwa kukamilika mwaka 2022, unatekelezwa katika vijiji saba kwenye wilaya saba nchini ukiwa chini ya Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) uliofadhiliwa na Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC).

# Museveni asema ADF wajisalimishe

**Kampala, UGANDA**

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, anasema kundi la waasi, Allied Democratic Forces (ADF), linastahili kujisalimisha, huku akisisitiza serikali yake imejitolea kukabiliana na ugaidi.

Katika hotuba iliyorushwa moja kwa moja kwenye televisheni siku tano, baada ya shambulio dhidi ya mji mkuu wa Kampala, Museveni alisema ADF wamejiamini.

Alisema wanajiamini sana kwa sababu wanaweza kutembea huru katika kambi za kijeshi nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na wanakojishughulisha na uchimbaji madini na biashara za mbao.

Hata hivyo alisema, Uganda itaendelea kuwasaka wanachama wa kundi hilo na kuongeza kuwa ni vyema wale ambao hawajasalimisha silaha zao wafanye hivyo.

Islamic State (IS), lilidai kuhusika na shambulio la Jumanne wiki iliyopita, ambalo lilisababisha vifo vya watu wanne na kuwajeruhi zaidi ya 30.

ADF katika miaka ya hivi karibuni na pia inajulikana kama Mkoa wa Afrika ya Kati ya Islamic State.

Museveni alisema, ADF sasa wamegeukia vitendo vya ugaidi katika maeneo ya mijini baada ya kushindwa katika eneo la Rwenzori na vijijini mwaka 2007.

Tangu Juni baada ya jaribio la mauaji ya waziri wa ngazi ya juu yanayoshukiwa kutekelezwa na waasi wa ADF, mashirika ya usalama ya Uganda, yamewaua washukiwa 12 na kuwakamata wengine 106.

Miongoni mwa watano kati ya wale waliouawa ni mhubiri wa Kiislamu aliyefariki siku tano zilizopita.

Rais Museveni kwa sasa anafanya mazungumzo na mwenzake wa DRC, Felix Tshiekedi juu ya uwezekano wa kupeleka wanajeshi wa Uganda Mashariki mwa DRC, kupambana na kundi la waasi.

Kikundi cha ADF, kilianzishwa Magharibi mwa Uganda, kiliundwa na wanajeshi waliokuwa wakimuunga mkono rais wa zamani wa nchi hiyo Idi Amin, na kuanzisha vita vya kupambana na utawala wa rais wa sasa, Museveni, kikidai utawala wake umekuwa ukiwafanyia maasi.

Kikundi hicho, kiliposhindwa na Jeshi la Uganda mwaka 2001, kilihamia katika Kivu ya Kusini, DRC.

Baada ya kipindi kirefu cha kusitisha harakati zake, ADF ilisikika tena mwaka 2014, ilipoanza mashambulio ya mara kwa mara dhidi ya raia wa DRC.

Mwaka 2015, Musa Seka Baluku alipochukua uongozi wa kundi hili baada ya mtangulizi wake Jamil Mukulu, kukamatwa na Bakulu kutangaza kujiunga na IS mwaka 2016.

**BBC**



Waziri Mkuu wa Sudan, Abdalla Hamdok, aliyeondolewa mamlakani baada ya mapinduzi ya ghafla ya kijeshi mwezi uliopita.

# Jeshi lakiri kumrejesha Hamdok madarakani

**Khartoum, SUDAN**

WAZIRI Mkuu wa Sudan, aliyeondolewa madarakani, Abdalla Hamdok anatarajiwa kurejeshwa kwenye madaraka, baada ya kuwekwa katika kifungo cha nyumbani wakati wa mapinduzi ya ghafla ya kijeshi mwezi uliopita.

Wafungwa wote wa kisiasa, pia wataachiliwa huru, kama sehemu ya makubaliano mapya kati ya wanajeshi, viongozi wa kiraia na makundi ya waasi wa zamani, wapatanishi walisema.

Oktoba 25, jenerali wa kijeshi wa Sudan, alitangaza hali ya hatari na kuvunja uongozi wa kiraia.

Ilizua maandamano makubwa ya wiki kadhaa, ambayo yalisababisha vifo vya watu wengi.

Makubaliano hayo, yaliafikiwa Jumamosi usiku, na yatatiwa saini ya utekelezaji baadaye, Mkuu wa Chama cha Umma cha Sudan, Fadlallah Burma Nasir, alithibitisha.

Hamdok amekubali masharti ya kukomesha umwagaji damu zaidi, shirika la habari la Reuters liliripoti, likinukuu chanzo kilicho karibu naye.

Kundi la wapatanishi, ambalo lilijumuisha wasomi, wanahabari na wanasiasa, lilitoa taarifa inayoeleza masharti ya mkataba huo.

Lilisema, Hamdok na wajumbe wake wa baraza la mawaziri ambao walizuiliwa wakati wa mapinduzi wataachiliwa na atarejea katika nafasi yake kama waziri mkuu.

Pia sheria zinazotawala mpito wa Sudan, kuelekea demokrasia zitarejeshwa.

Viongozi wa kijeshi na raia wa Sudan, wamekuwa katika mpangilio wa kugawana madaraka tangu Agosti 2019, baada ya rais wa muda mrefu wa kimabavu wa nchi hiyo, Omar al-Bashir, kupinduliwa.

Mpangilio huo uliingia katika mgogoro mwezi uliopita wakati kiongozi wa kijeshi, Jenerali Abdel Fattah Abdelrahman Burhan, alipovunja mkono wa kiraia wa serikali na kuwakamata viongozi wake.

Alisema hayakuwa mapinduzi, ni hatua inayohitajika kuzuia vita vya wenyewe kwa wenyewe, ambavyo vinatishia kuzuka kwa sababu makundi ya kisiasa yamekuwa yakichochea raia dhidi ya vikosi vya usalama.

Alijiteua mwenyewe kama mkuu wa baraza jipya tawala na viongozi wa kijeshi na waasi wa zamani wakiwa upande wake.

Katika miji mingi, ukiwamo mji mkuu Khartoum, waandamanaji wanaopinga mapinduzi waliweka vizuizi vya muda na mirundo ya matairi, wakiwa na hasira kwamba njia yao ambayo tayari ni tete ya demokrasia imetekwa nyara.

Jeshi lilijibu kwa ukali na linashutumiwa kwa kuwapiga risasi waandamanaji.

Makubaliano hayo mapya, yanakuja kabla ya mikutano zaidi iliyopangwa kufanyika.

**BBC**

# Sekunde 24 ya kifo ajali barabarani

**New York, MAREKANI**

WAKATI kila Novemba 21, maalumu kwa ajili ya kukumbuka waliopoteza maisha au kujeruhiwa kutokana na ajali za barabarani, Umoja wa Mataifa (UN), umesema kila sekunde 24 mtu mmoja anakufa kwenye ajali.

Ujumbe wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, katika maadhimisho jana, alisema ni wakati wa kutafakari juu ya vifo vilivyosababishwa na ajali za barabarani.

"Mtu mmoja katika kila sekunde 24 ina maana watu takribani watatu katika dakika moja na jumla ya watu 72 kwa siku nzima ya saa 24.

"Mwaka huu maudhui yanamulika umuhimu wa kupunguza mwendokasi barabarani ili kuzuia vifo na majeraha, hususan miongoni mwa vijana wa kike na wa kiume pindi wanapokuwa ndio kwanza wameanza maisha yao ya utu uzima pia watembea kwa miguu na watu wenye ulemavu."

Guterres alitoa wito kwa kila nchi, kampuni na raia kusaidia juhudi za kitaifa na kimataifa za kuhakikisha barabara zinakuwa salama zaidi, hususan kwenye nchi za kipato cha chini na kati ambako zaidi ya asilimia 90 ya vifo vitokanavyo na ajali barabarani hutokea.

Alisihi pia nchi wanachama wa UN, kuridhia mikataba ya kimataifa ya usalama barabarani na kutekeleza mipango kazi yote ya utekelezaji.

Kwa wahisani, alitoa wito waimarishe michango yao ya kifedha na kiufundi kupitia mfuko wa UN wa usalama barabarani.

"Tunapotazamia mkutano wa mwaka ujao wa ngazi ya juu wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, kuhusu mbinu za kuimarisha usalama barabarani, hebu na tukumbuke kuwa kila mmoja wetu ana jukumu la kufanya, ili barabara zetu ziwe salama. Leo na kila siku tuazimie barabara ziwe salama kwa kila mtu kokote aliko."

Siku ya kukumbuka waliokufa au waliojeruhiwa kutokana na ajali za barabarani, inatokana na azimio namba 60/5 la Desemba Mosi, mwaka 2005 lililopitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, huku mwaka 2020 UN, ikitangaza muongo mmoja wa kuimarisha usalama barabarani kuanzia mwaka 2020 hadi 2030.

**UN**

# YANGA UKIKAMATA WAWILI TU KWISHA KAZI - NAMUNGO

**Na Adam Fungamwango**

MENEJA wa Namungo FC, John Wiliiam 'Del Piero', ametoa siri ya ubora wa Yanga kwa sasa kuwa ni wachezaji wake wawili wa kiungo, Yannick Bangala na Feisal Salum kuwa ndiyo wanaoiendesha timu na kama ukiwawekea mikakati ya kuwazuia, basi unakuwa umeimaliza.

Akizungumza baada ya mechi kati ya timu yake dhidi ya Yanga iliyopigwa Uwanja wa Ilulu mjini Lindi na timu hizo kutoka sare ya bao 1-1, meneja huyo alisema kuwa wakati wa kujiandaa na mechi dhidi ya Yanga walikuwa wakiangalia nguvu yao ilipo pamoja na mapungufu yao, hivyo wakagundua kuwa Bangala na Fei Toto ndiyo wanaoiendesha timu.

"Tukaambizana tukate mawasiliano, tuhakikishe hawatembei, hawafanyi huduma yoyote kwa washambuliaji ndiyo maana uliona mbele kama kumekufa na sisi ndiyo tumeingia zaidi kwenye eneo la hatari zaidi kuliko wao, ukikata mawasiliano ya Bangala na Fei Toto Yanga inakuwa ya kawaida tu," alisema meneja huyo.

Mchezaji aliyekosa mabao mengi ya wazi kwenye mechi hiyo, Shiza Kichuya yeye alisema kuwa waliwakamata Yanga kila eneo na kila shabiki aliyeshuhudia mechi hiyo ameona kilichotokea.

"Sisemi kama tumeonewa, kwa sababu nikisema hivyo nitafungiwa, lakini kila mtu ameona, tumewashika Yanga kila eneo, lakini kilichotokea kila mtu ameshuhudia," alisema.

Naye mfungaji wa bao, Obrey Chirwa alisema wala haoni ajabu kufunga bao dhidi ya Yanga, kwa sababu ameshawafunga hata akiwa na Azam FC.

"Yanga siyo timu mbaya na ina wachezaji wazuri, lakini wanatakiwa wajiongeze tu, mimi kwangu kuwafunga si jambo la ajabu tena, ni kawaida, huwa nawafunga sana hata nikiwa Azam FC," alisema Chirwa ambaye aliwahi kuichezea Yanga.

Wakati Chirwa akiifungia Namungo, Saido Ntibazonkiza, aliiisawazishia Yanga kwa mkwaju wa penalti iliyozua malalamiko mengi.



Mkuu wa Kitengo cha Bia ya Serengeti Lite wa Kampuni ya SBL, Nandi Mwiyombella (kulia), akimkabidhi mmoja wa washindi wa shindano la kusaka vipaji vya Madj, Dj Son kutoka mkoani Kilimanjaro, sehemu ya zawadi ya seti ya vifaa vya kupiga muziki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serengeti Lite yapata washindi shindano la Madj

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya miezi mitatu ya mchakamchaka wa nchi nzima kutafuta Madj wachanga wenye vipaji, mchakato huo sasa umekamilika kwa kuwapata watatu wakali zaidi walioibuka vinara kufuatia mchujo mkali uliowezeshwa na Bia ya Serengeti Lite kupitia kampeni ya 'Take a Bite Out of Life'.

Abdulaziz Juma maarufu kama Dj Dully kutoka Dodoma ndiye aliyeibuka kinara katika fainali zilizofanyika jijini Arusha huku akifuatiwa na Steven Jonathan maarufu kama Dj Stegio kutoka Dar es Salaam na nafasi ya tatu ikichukuliwa na Musa Shabani maarufu kama Dj Son kutoka mkoani Kilimanjaro.

Miamba hiyo, iliibuka mshindi baada ya mchujo mkali uliohusisha Madj 21 wakali kutoka kila kona ya nchi ambapo mchujo mkali ulifanyika na kupatikana Madj saba na baadaye vinara watatu.

Shindano hilo kubwa zaidi kuwahi kufanyika hapa nchini kwa ajili ya kusaka vipaji vya Madj chipukizi, liliandaliwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kupitia bia yake ya Serengeti Lite, kupitia kampeni "Take a Bite out of Life', inayowahamasisha vijana na wateja wake kujiongeza, kufanya zaidi huku ikitoa fursa ya wenye vipaji kuonyesha uwezo wao na kuwaandaa kuwa wanachotaka.

Kampeni hiyo ililenga kuwafanya wateja wa Serengeti Lite kufurahia ladha ya kipekee ya bia hiyo ya Kitanzania, iliyotengenezwa Tanzania kwa ajili ya Watanzania huku wakionyesha vipaji na uwezo wao.

Kwa mujibu wa Meneja Mwandamizi wa Chapa wa Serengeti, Wankyo Marando, kampeni hiyo ilikuwa ni maalum kwa watu na vijana wenye uthubutu, wanaojiongeza na ambao wanafanya zaidi na zaidi ili kufikia malengo waliyojiwekea bila woga wala kuangalia nyuma.

Jumla ya washiriki zadi ya 5,000 kutoka shehemu mbalimbali nchini walipata jukwaa la kuonyesha vipaji vyao na washindi watatu walipata zawadi ya vifaa vya Madj vyenye thamani ya hadi shilingi milioni saba kila moja huku wakipewa nafasi za kufanya kazi kama Madj wa Serengeti Lite katika sehemu wanazoishi.

Washiriki ambao hawakuweza kufika fainali, walipata zawadi mbalimbali kama baketi za bia, tisheti, kofia pamoja na kupata jukwaa la kuonyesha vipaji vyao chini ya chapa ya bia inayoheshimika na kupendwa, Serengeti Lite.

Akizungumza wakati wa kuwakabidhi zawadi washindi watatu, Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa la Taifa, Matiko Mniko, aliishukuru Serengeti Lite kwa kuweza kuwapa vijana jukwaa la kuonyesha vipaji vyao.

"Washiriki wote wameonyesha uwezo mkubwa lakini hawa watatu wameonyesha uwezo mkubwa zaidi. Kikubwa hapa tumewaona pamoja na uwezo wao na hii ni hatua mojawapo ya kufikia mafanikio," alisema.

# Ligi ya Rugby yaja

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Chama cha Mchezo wa Raga (Rugby) nchini Tanzania umesema uko kwenye mikakati ya kurejesha hamasa kwa kuanzisha ligi mapema mwakani ili kutoa nafasi kwa watu kuanza kuufutilia mchezo huo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Rugby Tanzania, Jacob Jonas, alisema lengo lao kubwa ni kurejesha mchezo huo katika ramani nchini baada ya kulipotea kwa muda mrefu.

Alisema wamefanikiwa kuanzishwa kwa klabu kutoka mikoa saba kupata usajili wa timu kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ambalo limekitaka chama hicho kuandaa ligi na michuano mbalimbali.

"Tayari tumeanza kutambulisha mchezo huu na tumeandaa mashindano ya Taifa yaliyomalizika juzi na mikoa mbalimbali ilishiriki ikiwamo wenyeji Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Dodoma, Zanzibar na Tanga, mashindano hayo ni kuonyesha serikali kuwa tumedhamiria kurudisha mchezo huu kwenye ramani," alisema Jacob.

Alisema walipokea ujumbe kutoka BMT baada ya kusajili klabu na kuandaa mashindano sasa wanatakiwa kusajili chama chao na kuandaa ligi kwa kushirikisha timu zote ambazo zinatambulika na baraza hilo.

Mwenyekiti huyo alisema mpango mwingine ni kuhakikisha wanaendelea kufanya usajili wa kutembelea katika mikoa mingine ili kupata timu nyingi na kurejesha mchezo huo katika ngazi ya kitaifa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### UNITED KUMSHAWISHI ZIDANE
MANCHESTER United inaangalia uwezekano wa kumshawishi kocha wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane kuchukua nafasi ya kuinoa timu hiyo. United ipo kwenye harakati za kutaka kumfukuza kocha wake wa sasa, Ole Gunnar Solskjaer hapo Old Trafford. **(Times)**

### STERLING AITAKA BARCA
WINGA wa Manchester City na England, Raheem Sterling ameiambia klabu yake kwamba, anataka kwenda kwa mkopo Barcelona wakati wa dirisha dogo la Januari. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ameanza katika mechi tatu tu msimu huu hapo City. **(90 min)**

### ADEYEMI MBADALA WA LACAZETTE
ARSENAL inaangalia uwezekano wa kumsajili kinda wa RB Salzburg, Karim Adeyemi. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 raia wa Ujerumani, anatajwa kwenda kuchukua mikoba ya Alexandre Lacazette. **(Mirror)**

### DEMBELE ATAKIWA UNITED
MANCHESTER United ina nia ya kutaka kumsajili winga wa Barcelona, Ousmane Dembele. Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 24, ataangia miezi sita ya mwisho kwenye mkataba wake wiki zinazokuja, huku United ikionyesha nia ya kumtaka. **(Mundo Deportivo)**

### LINGARD KUONDOKA MAN U
JESSE Lingard anataka kuondoka Manchester United wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, mazungumzo yake na Man United yalivunjika hivi karibuni. **(Mirror)**

### LAMPARD KUMRITHI RODGERS
KLABU ya Leicester imemtambua kocha wa zamani wa Chelsea, Frank Lampard kama ndiye mtu anayefaa kumrithi Brendan Rodgers ambaye anaweza kutimuliwa baada ya timu hiyo hivi sasa kuwa nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England. **(Fichajes)**

### SPURS YAMTAKA DE LIGT
KLABU ya Tottenham Hotspur imemfanya mlinzi wa Juventus na Uholanzi, Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 22, kuwa chaguo lao la kwanza katika usajili wa Januari. **(Football Insider)**

### TUCHEL AMTAKA GALLAGHER
KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel anataka kufanya mazungumzo kuhusu kumchukua kiungo wa Crystal Palace, Conor Gallagher kwa mkopo. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, amefunga mabao manne na kutoa pasi za mwisho 10 kwenye Ligi Kuu msimu huu. **(Four Four Two)**

### PSG HAINA MPANGO NA HAALAND
KLABU ya Paris St-Germain imeaachana na mpango wa kuwania kumsajili straika wa Norway na Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21. **(El Nacional)**

### WINKS AWANIWA NEWCASTLE
KIUNGO wa England, Harry Winks anawaniwa na Newcastle huku kocha, Eddie Howe akimtaka mchezaji huyo katika usajili wa Januari. Winks mwenye umri wa miaka 25, ameanza katika mechi moja tu kwenye Ligi kuu England akiwa na Tottenham msimu huu. **(Mail)**

### BAYO ATAKIWA WEST HAM
WEST Ham inajiandaa kutoa ofa ya pili kwa straika wa Clermont, Mohamed Bayo mwenye umri wa miaka 23. **(Sun)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AGUERO RASMI SASA KUTUNDIKA DALUGA

●●●Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, ataachana na mchezo huo aliojihusisha nao kwa kipindi cha miaka 18, kutokana na matatizo ya...

**BARCELONA, Hispania**

STRAIKA wa Barcelona na gwiji wa zamani wa Manchester City, Sergio Aguero anatarajia kustaafu rasmi soka wiki hii, kwa mujibu wa ripoti za kimatibabu kutoka nchini Hispania.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, ataachana na mchezo huo aliojihusisha nao kwa kipindi cha miaka 18, kwa sababu ya matatizo ya moyo aliyoyapa kwenye mchezo wake wa kwanza wa LaLiga pale Camp Nou.

Straika huyo wa zamani wa Man City, alipata tatizo hilo wakati wa mchezo wa sare ya bao 1-1 nyumbani dhidi ya Alavés mwanzoni mwa Novemba na ilionekana kwamba raia huyo wa Argentina angekaa benchi kwa miezi mitatu.

Hata hivyo, kwa mujibu wa mwandishi wa habari za michezo, Gerard Romero, Aguero sasa atatakiwa kustaafu baada ya vipimo kuonyesha kwamba, hataweza kuendelea kucheza kutokana na tatizo hilo.

Kwa mujibu wa Romero, mwandishi maarufu zaidi wa michezo Ulaya, tangazo rasmi la kustaafu kwa Aguero litafanyika wiki hii.

Mashabiki wa Man City pia watashtushwa sana na taarifa hizo baada ya kucheza pale kwenye Uwanja wa Etihad takriban muongo mmoja, tangu alipojiunga nayo akitokea Atletico Madrid kipindi cha majira ya joto mwaka 2011.

Katika mashindano yote, amecheza mechi 390 kwa Man City, akifunga mabao 260 na asisiti 73 na kushinda mataji 15.

Aguero alisajiliwa Barcelona katika usajili huru baada ya kumaliza muda wake wa uchezaji kule Man City.

MECHI KALI
HOME AWAY
VERONA
1.74 | 4.01 | 4.21
EMPOLI

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO



# MAN UNITED YAMFUTA KAZI SOLSKJAER

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imemfuta kazi kocha wake Mkuu, Ole Gunnar Solskjaer kufuatia kipigo cha mabao 4-1 ilichokipata dhidi ya Watford juzi, Jumapili.

United imeshinda mchezo mmoja tu kati ya saba iliyopita ya Ligi Kuu England na ipo katika nafasi ya saba kwenye msimamo huku ikiwa pointi 12 nyuma ya vinara wa ligi hiyo, Chelsea.

Kocha wa kikosi cha kwanza, Michael Carrick ndiye amepewa nafasi hiyo kwa muda wakati United ikisaka kocha wa muda kumalizia msimu huu.

"Ni masikitiko kwamba tumefikia maamuzi haya magumu," United imeeleza.

Hivi karibuni United ilipata matokeo mabaya ikiwa ni pamoja na kichapo cha mabao 5-0 dhidi ya Liverpool Oktoba 24 na kile cha mabao 2-0 dhidi ya Manchester City Novemba 6, mwaka huu.

United iliongeza: "Wakati wiki chache zilizopita zimekuwa zakukatisha tamaa, haziwezi kuficha kazi zote alizozifanya katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita za kujenga upya misingi ya mafanikio ya muda mrefu.


"Ole anaondoka na shukrani zetu za dhati kwa juhudi zake bila kuchoka kama kocha na tunamtakia kila la heri kwa siku zijazo.

"Nafasi yake katika historia ya klabu itakuwa salama kila wakati, si tu kwa hadithi yake kama mchezaji, lakini kama mtu mashuhuri na kocha ambaye alitupa wakati mwingi mzuri. Atakaribishwa milele Old Trafford kama sehemu ya familia ya Manchester United."

Darren Fletcher ataendelea kubaki kama mkurugenzi wa ufundi, wakati Mike Phelan na Kieran McKenna - ambao walikuwa sehemu ya benchi la ufundi la Solskjaer, pia watabakia klabuni hapo kwa muda huu.

Mechi ijayo ya United itakuwa ugenini nchini Hispania kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Villarreal Jumanne kabla ya kurejea kwenye ligi kucheza dhidi ya Chelsea na Arsenal.

# Messi afunga bao la kwanza Ligue 1



**PARIS, Ufaransa**

LIONEL Messi amefunga bao lake la kwanza kwenye Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, kwa klabu yake ya Paris Saint-Germain, juzi Jumamosi wakati wakiifunga Nantes mabao 3-1.

Bao hilo ambalo lilikuwa la tatu kwa PSG, limewafanya kuongoza msimamo wa ligi hiyo kwa tofauti ya pointi 13 kileleni.

Messi alifunga bao hilo kwa mguu wa kushoto ndani ya eneo la penalti zikiwa zimebakia dakika tatu mpira kumalizika.


Bao hilo lilikuwa la tatu kwa PSG baada ya Dennis Appiah kujifunga na kuwa bao la pili baada ya Randal Kolo Muani kusawazisha lile la ufunguzi la Kylian Mbappe.

Matokeo hayo yamewafanya PSG kufikisha pointi 37 baada ya kucheza mechi 14 na wanakabiliwa na mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester City Jumatano, huku Nantes wakiwa nafasi ya 11 na pointi zao 18.

Messi amefunga mabao matatu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu alipojiuga na klabu hiyo akitokea Barcelona na raia huyo wa Argentina hakufunga kwenye ligi katika mechi zake tano alizocheza.

LIVE IN PLAY

# KLOPP ATOA SABABU KUMVAA ARTETA



**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp ameelezea kwa nini alimvaa Mikel Arteta kwa sababu raia huyo wa Hispania pamoja na benchi lake la ufundi walitaka Sadio Mane atolewe nje kwa kadi nyekundu, huku Liverpool ikishinda 4-0 dhidi ya Arsenal, Jumamosi.

Mane, ambaye amefunga mabao mengi ya Ligi Kuu dhidi ya Crystal Palace (13) huku Arsenal akiwafunga mara nane, alifunga la ufunguzi kipindi cha kwanza pale kwenye dimba la Anfield, kabla ya Diogo Jota, Mohamed Salah na Takumi Minamino kila mmoja kufunga moja na kujivuta hadi nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi.

Mshambuliaji huyo wa Senegal alifunga bao kwa kichwa muda mchache baada ya makocha hao wawili kutupiana maneno, kwa sababu Mane alionekana kumfanyia faulo, Takehiro Tomiyasu.

Arteta na wasaidizi wake walighadhabika na walipaza sauti kwa mwamuzi kwamba, Mane alimpiga kiwiko mlinzi huyo wa Arsenal.

Klopp naye akajibu mashambulizi kabla ya mwamuzi, Michael Oliver kuingilia kati na kuwaonyesha kadi ya njano makocha wote wawili.

Alipoulizwa kuhusu tukio hilo baada ya mchezo huo, Klopp aliiambia Sky Sports: "Ilikuwa ni tukio ambapo Sadio hakufanya faulo, lakini benchi la Arsenal liliamka na kutaka itolewe kadi nyekundu. Niliwauliza wanataka nini kwenye tukio lile.

"Tulilazimika kumtoa Sadio nje kwenye mchezo dhidi ya Atletico (Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya) kwa sababu nao walitaka apewe kadi ya njano.

"Kwa hakika mwamuzi alifanya vizuri kwenye hali ile, ilistahili kadi ya njano."

# Muller afikisha mechi 600 Bayern



**MUNICH, Ujerumani**

THOMAS Muller amekuwa mchezaji wa kwanza kufikisha mechi 600 kwa Bayern Munich tangu kuundwa upya kwa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, mwaka 1963 baada ya kucheza dhidi ya Augsburg, Ijumaa.

Muller alikulia katika akademi ya Bayern na alichezeshwa mchezo wake wa kwanza wa Bundesliga na Jurgen Klinsmann Agosti mwaka 2008, lakini alicheza mechi nne tu kati ya 34 msimu huo.

Kuwasili kwa Louis van Gaal kulimpa nafasi Muller msimu wa 2009-10 akipata nafasi ya kucheza mara kwa mara kwenye kikosi hicho.

Msimu huu tayari amehusika katika mabao 17 kwenye Bundesliga akipitwa na Mohamed Salah pekee kwa bara la Ulaya aliyehusika kwenye mabao 20.

Katika umri wake wa miaka 32, Muller sasa anaiwania rekodi ya kuwa mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi kwa Bayern, ambayo iliwekwa na golikipa, Sepp Maier aliyecheza mechi 700.

SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA



PAKUA SASA

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 22 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:45 | 2495 | Machine Sazi Tabriz vs Esteghlal Khuzestan | 13.45 | 4.71 | 1.23 |
| 13:45 | 3154 | Arman Gohar Sirjan vs Ghasghaei Shiraz | 1.81 | 3.08 | 4.52 |
| 13:45 | 3373 | Rayka Babol vs Vista Turbine | 2.38 | 2.85 | 3.04 |
| 13:45 | 4689 | Saipa Karadj vs Khosheh Talaei | 2.03 | 2.83 | 3.94 |
| 14:15 | 2518 | Esteghlal Mollasani vs Shahrdari Astara | 2.04 | 2.94 | 3.71 |
| 14:15 | 3277 | Shahin Bushehr vs Pars Jonoubi Jam | 1.95 | 2.94 | 4.05 |
| 14:15 | 3658 | Agrobiznes Volochisk vs Polissya Zhytomyr | 3.37 | 2.98 | 2.14 |
| 15:00 | 2156 | Backa Palanka vs FK Zeleznicar Pancevo | 2.83 | 2.83 | 2.54 |
| 15:00 | 2872 | FK Graficar Beograd vs FK Kabel Novi Sad | 1.33 | 4.25 | 8.70 |
| 15:00 | 2922 | Indjija vs Javor Ivanjica | 2.27 | 2.99 | 3.09 |
| 15:00 | 5308 | Pescara Youth vs Hellas Verona Youth | 3.19 | 3.53 | 1.99 |
| 15:05 | 2990 | Alshoulla vs AL Jeel | 2.00 | 3.08 | 3.61 |
| 15:20 | 4459 | Al Jabalain vs Ohud Medina | 1.58 | 3.62 | 5.21 |
| 15:30 | 1024 | DAR AL Dawa vs Kfarsoum | 2.29 | 3.17 | 2.88 |
| 16:00 | 2869 | ES Hammam Sousse vs US Tataouine | 2.65 | 2.65 | 2.89 |
| 16:00 | 2916 | Avenir Rjich vs AS Slimane | 2.19 | 2.79 | 3.51 |
| 16:00 | 2936 | Olympique de Beja vs ES Sahel | 3.40 | 2.69 | 2.30 |
| 16:00 | 3234 | Ipswich U23 vs Millwall U23 | 1.95 | 3.66 | 3.18 |
| 16:00 | 4847 | Swansea U23 vs Charlton U23 | 1.86 | 3.77 | 3.38 |
| 16:45 | 3848 | Psis Semarang vs PSM Makassar | 2.65 | 3.09 | 2.51 |
| 17:00 | 2326 | Roma Youth vs Bologna Youth | 1.30 | 5.21 | 7.14 |
| 17:00 | 4264 | Cukaricki St vs Novi Pazar | 1.33 | 4.72 | 7.33 |
| 17:25 | 4190 | Al Khaleej Club vs AL Akhdood | 1.75 | 3.47 | 4.14 |
| 18:00 | 1514 | Esperance Tunis vs ES Metlaoui | 1.33 | 4.06 | 9.66 |
| 18:00 | 2928 | Hadiya Hosahina FC vs Adama City FC | 1.79 | 3.22 | 4.33 |
| 18:30 | 1075 | Levski Sofia vs Botev Vratsa | 1.30 | 4.73 | 8.30 |
| 18:30 | 2073 | CS Mioveni vs Gaz Metan Medias | 2.67 | 2.96 | 2.72 |
| 18:30 | 4321 | Alliance Lypova Dolyna vs VPK Agro Magdalinovka | 1.61 | 3.77 | 4.64 |
| 18:45 | 2903 | Din. Tirana vs Egnatia Rrogozhine | 1.62 | 3.46 | 5.19 |
| 19:00 | 1492 | Lamia vs Panathinaikos | 3.75 | 3.26 | 1.99 |
| 19:00 | 1521 | Apollon Limassol vs Paeek | 1.22 | 5.92 | 11.85 |
| 19:00 | 5924 | Eyupspor vs Samsunspor | 2.41 | 3.33 | 2.60 |
| 20:00 | 2365 | Sandecja vs Widzew Lodz | 2.66 | 3.24 | 2.41 |
| 20:00 | 2480 | Zaglebie Lubin vs Radomiak Radom | 2.45 | 3.18 | 2.65 |
| 20:00 | 4593 | Kayserispor vs Goeztepe | 2.46 | 3.32 | 2.72 |
| 20:00 | 5869 | Trabzonspor vs Gaziantep BB | 1.55 | 4.30 | 5.60 |
| 20:30 | 2448 | Veres Rivne vs FC Metalist 1925 | 2.23 | 3.28 | 2.89 |
| 20:30 | 5205 | Verona vs Empoli | 1.74 | 4.01 | 4.21 |
| 21:00 | 1179 | Norrkoping vs Djurgardens IF | 2.70 | 3.28 | 2.35 |
| 21:00 | 2003 | AEK Larnaca vs Apoel Nicosia | 2.34 | 3.26 | 2.97 |
| 21:00 | 2118 | Sonderjyske vs Aalborg | 3.30 | 3.39 | 2.10 |
| 21:00 | 2970 | Meppen vs Viktoria Koln | 2.07 | 3.53 | 3.19 |
| 21:00 | 3799 | Orebro SK vs Kalmar | 4.62 | 3.71 | 1.63 |
| 21:00 | 5587 | Real Sociedad B vs Girona | 2.56 | 3.00 | 2.81 |
| 21:30 | 2447 | Zulte Waregem U21 vs Mechelen U21 | 1.65 | 4.05 | 4.05 |
| 21:30 | 3682 | Anderlecht U21 vs KAA Gent U21 | 1.82 | 4.10 | 3.80 |
| 21:30 | 4392 | AS Eupen U21 vs Excelsior Virton U21 | 1.39 | 5.01 | 5.58 |
| 21:30 | 4818 | Voluntari vs Dinamo Bucuresti | 1.87 | 3.43 | 3.92 |
| 21:30 | 4905 | St Truiden U21 vs Cercle Brugge U21 | 3.02 | 3.79 | 1.98 |
| 21:30 | 5382 | Kortrijk U21 vs Westerlo U21 | 3.23 | 3.66 | 1.94 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Novemba 22, 2021

Nipashe




Aguero rasmi sasa kutundika daluga

UKURASA 21

HESHIMA....




Baadhi ya viongozi wa Simba na mgeni rasmi wa mkutano mkuu wa mwaka wa klabu hiyo, Musa Azan Zungu (kulia), wakiwa wamesimama wakati wa wimbo wa Taifa ukiimbwa. Mkutano huo ulifanyika Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Nabi alia uwanja, Kaze atoa mbinu

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, akisema Uwanja wa Ilulu mjini Lindi ulisababisha washindwe kucheza soka lao lililozoeleka na kusababisha sare ya bao 1-1 dhidi ya Namungo FC juzi, Kocha Msaidizi Cedric Kaze amesema kuwa inabidi sasa waandae wachezaji wao wawe na uwezo wa kucheza kwenye aina zote za viwanja kama wanahitaji kupata ubingwa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baada ya mechi ya Ligi Kuu raundi ya sita kati ya timu hizo kutamatika, Nabi alisema haikuwa rahisi kwao kucheza mpira mzuri kama kawaida yao na kupata matokeo mazuri kwenye hali ile ya uwanja wa Ilulu jinsi ilivyokuwa.

Hata hivyo, aliwasifu Namungo kuwa walicheza kwa kupambana, nayo pia ilichangia wao kutopata matokeo mazuri kwenye mechi hiyo.

"Siyo rahisi kucheza mpira wetu mzuri kwenye uwanja kama huu, lakini hiyo siyo sababu pekee, pia Namungo walipambana pia, japo uwanja ulikuwa hausapoti pasi," alisema Nabi.

Kwa upande wa Kaze, alisema ni kweli uwanja haukuwa mzuri, lakini na wao pia hawakucheza vema kwenye mechi hiyo, huku baadhi ya wachezaji hasa wapya wakionekana waoga kutokana na uwanja jinsi ulivyokuwa.

# CHAMA AIBUKA MKUTANO SIMBA

## ●●●Mabilioni yatumika, Mo Dewji apewa urais huku Yanga ikitangaziwa maumivu makali baada ya...

**Na Saada Akida**

MASHABIKI wa Klabu ya Simba wametakiwa kutokuwa na hofu wala kukubali kukosa usingizi juu ya kelele za wapinzani wao kwa kuwa uongozi wa timu hiyo unaweza kufanya usajili mkubwa ikiwa ni pamoja na kumrejesha kiungo fundi Mzambia Clatous Chama 'Mwamba wa Lusaka'.

Akizungumza katika Mkutano Mkuu wa klabu hiyo, Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again', alisema timu hiyo imerejea katika makali yake na muda si mrefu wataipita Yanga kama imesimama na kurejea katika nafasi yao ya kuongoza na kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tunayo jeuri hiyo kwa sababu Simba imewekeza katika soka na si maneno, fitna na vijembe huko tumeshapita kazi yetu kubwa ni kupambana uwanjani kuhakikisha wachezaji na viongozi kwa pamoja tunapata matokeo na kufikia malengo yetu."

"Maneno maneno tumeshapita, ukiangalia kwa sasa Simba ni miongoni mwa timu 10 bora za Afrika, niwaombe wanachama mna kila sababu ya kutembea kifua mbele, watake wasitake mpira tutacheza hata wakitubadilishia uwanja," alisema Try Again.

Aidha, Try Again, alisema bodi kwa kutambua mchango wa Mohamed "Mo" Dewji, aliwataka wanachama kuridhia agenda zilizopo ikiwamo mapato na matumizi ya fedha na mikakati iliyopo msimu huu, huku wakiridhia juu ya Mwekezaji Mohamed "Mo" Dewji kupewa urais wa heshima ndani ya klabu hiyo, lakini Kassim Dewji kuteuliwa kuwa mwenyekiti wa kamati ya usajili kuchukuwa nafasi ya Zakaria HansPope aliyetangulia mbele za haki.

"Mo Dewji kwa anayoyafanya bodi kupita ibara ya 50 kumpa urais wa heshima ni kwa sababu yupo na ataendelea kuwapo sana Simba na ameahidi kuendelea kuweka mabilioni kwa ajili ya usajili wa mchezaji yeyote hata kumrejesha Clatous Chama uwezo huo upo," alisema Try Again huku wanachama wakilipuka kwa shangwe.

Alisema viongozi wa Simba hawajalala na wana mikakati madhubuti, kwa kauli ya Mwenyekiti, Murtaza Mangungu na Mtendaji Mkuu, Barbara Gonzalez, wataendelea kutetea ubingwa wao kwa mara ya tano.

"Kwa sasa tunaenda kucheza michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, kwa ukomavu wetu tunaenda kutikisa tena Afrika baada ya hapo tunarejea kujiandaa na ligi na kuhakikishia kwamba Desemba 11, mwaka huu, hawatoki na tutashughulika siku hiyo.

"Niwahakikishie siku hiyo wakae vizuri tunajua mipango yote na kwa kuwa sisi ni wenyeji wa mchezo huo wajiandae kuzoea kufungwa, wamekwisha," alisema Try Again.

Alitoa wito kwa watumishi wa Simba kila mmoja kwa nafasi yake lazima afanye kazi yake kwa bidii ili kupata mafanikio ambayo yanatarajiwa na kila Mwanasimba.

Kuhusu mabadiliko ya klabu hiyo, alisema mchakato umefikia katika hatua nzuri baada ya kukamilika kwa upande wa serikali na mwekezaji kuweka bilioni 20, hivyo kazi iliyopo kwa sasa ni kufanya uhakiki wa wanachama.

Alisema tayari wameunda kamati inayoongozwa na Azizi Kifile akisaidiana na wajumbe wengine, akiwamo Mangungu, Mlamu Ng'ambi na Barbara kuhakikisha jambo hilo linaisha kwa haraka.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa klabu hiyo, Mangungu amebainisha kwamba klabu ina mpango wa kujenga ukumbi wa mikutano na ofisi kwenye jengo lao lililoko Kariakoo, Msimbazi.

"Awali jengo hili ambalo ni moja ya vitega uchumi vya klabu lilikuwa likiingiza Sh. milioni 200 kwa mwaka, lakini sasa linaingiza Sh. milioni 500, tumezungumza na mwekezaji ili klabu ijenge ofisi na ukumbi kwenye jengo hilo, mchakato utaanza Januari," alisema Mangungu.

Katika mkutano huo uliohudhuriwa na viongozi wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Shirikisho la Soka nchini (TFF), likiwakilishwa na Steven Mguto, huku mgeni rasmi akiwa Mbunge wa Ilala, Mussa Azan Zungu, ajenda 10 kati ya 11 zilizowasilishwa zilijadiliwa.

Mkuu wa Kitengo cha Fedha, Utawala na Utendaji wa Simba, Yusuph Nassor, alitoa mchanganuo wa fedha ikiwamo mapato na matumizi ya msimu uliopita na msimu huu.

"Kwa mwaka wa fedha wa 2020-21 vyanzo vya mapato ilikuwa Sh. bilioni 12.17 na mwekezaji aliweka bilioni 5.2 fedha hizo ni nje ya bilioni 20 ambazo zimeingizwa hivi karibuni, na matumizi yalikuwa Sh. bilioni 12.33.

"Kwa mwaka huu matumizi ni Sh. bilioni 11.8 huku Mo Dewji akiendelea kuweka bilioni 5.1 katika fedha hizo bilioni 1.2 zilizotumika katika usajili wa wachezaji waliongezwa msimu huu, kwa hatua hii lazima bajeti ya Simba iwe kubwa ili kuja kushindana na klabu kubwa ikiwamo Al Ahly ya Misri ambao bajeti yao inasimama kwenye bilioni 80," alisema Nassor.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042